ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Sita – Tarehe 2 Agosti, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwape taarifa kwamba kwa ratiba yetu wizara hii tunataka leo tufanye majumuisho na tumalize na huku juu, tayari kuna wachangiaji 6 ambao tutawapa nafasi na wakatapomaliza hao tutamwita Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho na baadaye tupitishe vifungu. Sasa wale wote ambao bado hawajaleta na wana nia wamuwahi Mhe. Waziri wapeleke michango yao kwa maandishi ili tuweze kwenda vizuri kwenye shughuli zetu.

Baada ya maelezo hayo, tunamwita Mhe. Abdalla Moh'd Ali, halafu Mhe. Asaa Othman Hamad atafuatia.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fursa ya kwanza leo hii siku ya Ijumaa kwa ajili ya kusema machache katika Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, ningeanza kidogo kwenye kujenga uwezo wa kitaalamu na waliotuandikia wamesema *possibility and barcode*. Mhe. Naibu Spika, ninachokifahamu kwamba mara nyingi watumiaji wa bidhaa huwa wanaangalia bidhaa ile ilipotengenezwa na kwa kumbukumbu zangu miaka ya nyuma ilikuwa zaidi tukinunua bidhaa ya shoka kutoka China, kwa sababu ndio tuliyokuwa tunaiona ina *durability* kubwa, lakini bidhaa nyingi ambazo zilikuwa zinatoka Jamhuri ya China tulikuwa tunazikataa kwa sababu *durability* au uwezo wake wa kukaa muda mrefu haupo.

Sasa wizara imetuambia kwamba imeanzisha utaratibu wa kuzipatia *bar code* bidhaa zetu za Zanzibar. Nafikiri hili ni suala zuri lakini kidogo nimepata wasi wasi kwamba nchi yetu inajulikana rasmi kwamba haina maendeleo yoyote yale ya viwanda. Kwa hivyo, bidhaa zetu tutakapokuwa tunazitia hii *barcode* ni kweli zitapata utambulisho na zitajulikana kwamba bidhaa hizi zinatoka nchi ya Zanzibar, lakini je bidhaa hizi zitakuwa zinapata soko. Mhe. Naibu Spika, nina wasi wasi zitakuwa hazina ubora kwa sababu tunajulikana kwamba sisi sio nchi ya viwanda.

Kwa hivyo, mimi nafikiri hapa labda tungeiachia bidhaa moja tu ya karafuu ndio itumie *barcode* hii, kwa sababu hizi bidhaa nyengine viwango vyake ni vidogo. Kutokana na hali hiyo, nina wasi wasi tutakapozitia *barcode* hii na zitakapokwenda nchi za nje zitakuwa zinajulikana kwamba *quality* yake ni ndogo, upatikanaji wa masoko pia utakuwa ni mdogo sana. Kwa upande mmoja ni kweli kwamba tutapata utambulisho na tutajulikana lakini je tutapata masoko.

Mhe. Naibu Spika, naomba kushauri tu kwamba hii *barcode* basi isitumike kwa bidhaa zote. Nadhani ni vyema tukaziachia bidhaa nyengine zikaingia katika soko kwa siri au kificho na kuliko kuzitambulisha rasmi, kwa sababu ukizitambulisha rasmi Mhe. Naibu Spika zitajuliakana, nafikiri hili kila mmoja analielewa. Kwa mfano, leo hii tunapokwenda madukani kutafuta bidhaa tunaiangalia inatoka nchi gani, kuna baadhi ya nchi tunazikataa na tunasema hazina ubora. Sasa nahofia na sisi tukaja tukakosa soko kwa bidhaa zetu. *(Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kidogo kwenye Mamlaka ya Vipimo ya Zanzibar na Kamisheni ya Ushindani. Kwa kweli hivi sasa ninachokijua Mhe. Naibu Spika ni kwamba Shirika letu la *ZSTC* limeanzisha utaratibu wa kuleta mezani za *digital* na ninafikiria kwa karne tuliyonayo hili ni jambo la busara. Vile vile hivi karibuni wizara inatarajia kutuletea Sheria ya Mezani na Sheria ya Ushindani pia huenda ikawekwa mezani hivi karibuni. Kwa hivyo, hivi sasa *ZSTC* tayari wameshaanzisha uletaji wa mezani za *digital*. Jee, katika sheria hii labda niulize tayari na utumiaji wa mezani hizo za *digital* katika maeneo mengine yasiyokuwa ya *ZSTC* zitatumika au bado tutaendelea kutumia mezani zetu zile za mawe za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni kwamba ripoti za Wizara ya Fedha zinaoneshwa kwamba *inflation* mwaka huu ilisababishwa na zao la samaki kupanda na kushuka. Kwa kweli hivi sasa bidhaa nyingi za vitoeleo zinapimwa na juzi tulikuwa tunazungumzia sana hapa bidhaa ya *PADUU* ile nyama ya kuku. Utaratibu uliopo ni kwamba kitoeleo kile tunatumia mezani.

Sasa ikiwa serikali imeona utaratibu uliopo hivi sasa wa uuzaji wa samaki ndio uliosababisha kupanda na kushuka kwa bei za bidhaa nyengine.

Mhe. Naibu Spika, labda niwaulize Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwamba kuna utaratibu wowote ule ambao umepangwa wa kuangalia labda na samaki na wao tutawaingiza katika utaratibu huu wa kuwapima, ili kuondosha ile *inflation* ya bei katika bidhaa nyengine ili kumlinda zaidi huyu mwananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, hii ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na ninachokumbuka ni kwamba tulikuwa na kiwanda kimoja kinachoitwa Sukari na Manukato na kiwanda hichi kilikabidhiwa mwekezaji karibu miaka mitatu. Pia tulikuwa na mawazo kwamba kufanyakazi kwa kiwanda hichi kungesaidia wananchi wetu kupata ajira pamoja na kupata sukari ambayo ina matumizi makubwa katika nchi hii na labda kupatikana kwa sukari katika nchi hii basi kungepunguza ule urari wa bei za sukari tulionao hivi sasa.

Hata hivyo mwaka jana tuliletewa ripoti na tukaambiwa kwamba serikali imeunda kamati za kufuatilia kwa nini kiwanda hichi hadi leo mwekezaji ameshindwa kuzalisha sukari. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba wizara inieleze jee, hadi hivi sasa serikali ina mtazamo gani kuhusu mwekezaji huyu aendelee kuekeza au anaondoka hasa tukitilia maanani kwamba katika sheria zetu tulizozipitisha hivi karibuni kuna sheria inayosema tunafuta kabisa *grace period*, yaani ule muda wa miezi 30 na huyu naye nahisi ameshapita muda huo.

Sasa hebu tuambieni kuna utaratibu gani ambao hivi sasa umefikiwa na serikali kuhusu mwekezaji huyu. Mhe. Naibu Spika, niende kidogo kwenye Shirika la *ZSTC* pamoja na Shirika la Magari. Kwanza ninachokijua kwamba upatikanaji wa zao hili kwa wingi uko katika Kisiwa cha Pemba lakini kwa mshangao ni kwamba wafanyakazi katika kisiwa kile wamepungua na hivi karibuni waliajiriwa vijana wasiopungua watatu lakini wakiwa na ngazi za *diploma*.

Vijana hawa kutokana na nafasi zinazotakiwa katika Kisiwa cha Pemba hawakukidhi haja inabidi kazi ziongezeke. Kwa hivyo, sijui kuna utaratibu mwengine ambao umepangwa wa kuwapeleka wafanyakazi ambao watakidhi au watajaza vizuri zile nafasi zilizopo.

Mhe. Naibu Spika, shirika hili hivi sasa linafanyiwa mageuzi na tunatarajia mageuzi haya yachukue miaka karibu 10 ili kumalizika na Shirika la Magari kwa taarifa zilizopo linataka kufungwa.

Shirika la *ZSTC* Mhe. Naibu Spika tuliandaa utaratibu maalum kwa ajili ya kulifufua na moja katika taratibu hizi ni kupunguza wafanyakazi. Kwa bahati nzuri kwamba wafanyakazi walipewa fursa ya kustaafu kwa hiari na Shirika la Biashara la Magari nalo pia linatarajiwa kufungwa wakati wowote.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, Shirika la *ZSTC* wao wamepewa fursa hii na kuna wafanyakazi wasiopungua 68 ambao wao wamekubali kustaafu kwa hiari. Sasa kama Shirika la Magari nalo tunao mpango wa kulifunga kwa nini na wao wasipewe fursa hii wakapata kustaafu kwa hiari na hivi sasa tunao kwenye shirika, hili ni mzigo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja labda anieleze kidogo kwa nini hawa na wao fursa hii wasipewe ya kustaafu kwa hiari zao, wakati shirika moja kwa moja limeshakusudiwa kufungwa.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa ofisi zetu zilizoko Dubai na Dar-es-Salaam na jana suala hili la ofisi hizi lilizungumzwa. Sasa ninachokijua ni kwamba hivi sasa karafuu zinahitajika na wala hakuna haja ya kutafuta soko huko ulimwenguni na wanaozihitaji wanakuja hapa Zanzibar na *technology* ya kileo inaturuhusu kupeleka bei na *sample* pahala popote pale unapohitaji. Kwa hivyo, hebu tuelezeni wizara kuna haja hivi sasa ya kuwa na ofisi zile pale Dubai na hata kama labda huyu ambaye yupo pale ametusaidia mambo mengine mbali mbali, lakini kuwepo kwake kunatusaidia nini sisi wakati *sampling* na *price* tunaweza kuzijua ndani ya dakika tano tu kwa *technology* yetu ambayo tunayo.

Lakini ofisi yetu ambayo ipo Dar-es-Salaam hivi sasa haitangazi zile bidhaa za karafuu na inauza zaidi bidhaa nyengine zisizokuwa za karafuu. Mhe. Naibu Spika, kuna umuhimu nao wa kuendelea kuwa na ofisi zile na labda hebu tuoneshwe mchanganuo kidogo wa mapato angalau turidhike. Jee, ofisi ile ina faida yoyote ambayo inayoingiza ndani ya shirika hili.

Mhe. Naibu Spika, naheshimu wakati wake, nashukuru.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante kwa mchango wako. Sasa nafasi tunampa Mhe. Asaa Othman Hamad, baadaye Mhe. Marina Joel Thomas na ajiandae Mhe. Ashura Sharif Ali.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia siku hii ya Ijumaa tukiwa

bado na idadi ile tuliyoondokea jana na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tukamilishe sala ya leo katika idadi hii.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu ni mdogo sana ambao utalenga kwenye ushauri kidogo na maswali ya hapa na pale.

Kwanza kama nilimsikia vizuri Mhe. Waziri wa wizara hii alitaja dhamira ya ujenzi wa ofisi yake kule Pemba. Kwa kweli hili ni jambo jema sana ni zuri ambalo tunalihitaji, isipokuwa nataka nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba utamaduni walioujenga viongozi tokea muasisi wa mapinduzi ya nchi hii na aliyefuatia Mhe. Rais wa awamu ya pili walijitahidi sana kuweka mambo kule Pemba kwa uwiano wa mikoa miwili iliopo, yaani Kusini na Kaskazini. Kutokana na hali hiyo, nitamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba aende na mstari huu kwamba kuitizama ofisi yake, stahili yake ibaki Kaskazini ama kama alipopataja yeye jana na ningemuomba sana hilo. *(Makofi).*

Pili Mhe. Naibu Spika, limetajwa sana na Waheshimiwa Wajumbe lakini kwa uzito wa jambo lenyewe ni kuhusu uingizwaji wa bidhaa *fake*. Kwa kweli hapa kuna bidhaa *fake* na uingizwaji wa bidhaa ambazo tayari zimeshatumika, nadhani ni mambo mawili tofauti.

Mhe. Naibu Spika, wote wawili hawa wanafanyabiashara au wanatafuta riziki zao, yaani mwenye kuingiza *fake* lakini huyu wa bidhaa *fake* ni mkorofi sana na huyu mwenye kuingiza *used* anataka taaluma. Mhe. Naibu Spika, hii ni ajira hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako kwamba hapa watendaji wajipange na umakini mzuri kidogo, ili tusije tukaathiri wenzetu ambao tayari wameshajipanga kwenye soko hili.

Lakini binadamu ni binadamu Mhe. Naibu Spika, tamaa mara nyingi inatutawala na kuna ugumu wake katika hili. Nadhani tufike mahala tuweke kiwango cha *used* kwamba tukubali kuingia nchini, lakini ni marufuku kabisa kuingiza *fake* na nafikiri tuwe wazi katika hili kwamba bidhaa *fake* hatuitaki kuingia nchini na bidhaa *used* tuiwekee kiwango kuingia hapa. Wananchi wetu hali zao kiuchumi ni ngumu na wala hawamudu kununua bidhaa mpya moja kwa moja kutoka madukani. Lakini pale atakapojitahidi angalau akaweza kununua bidhaa hiyo imsaidie kwa muda fulani, kwa hivyo ndipo nikataja kile kiwango.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nilitaka nije kwenye mazao ya biashara haraka haraka. Kwa kweli hapa Waheshimiwa Wajumbe wamezungumzia sana kwenye karafuu, nazi na Zanzibar tunaitaja kwamba ni *Spice Island*.

Sasa kwa maoni yangu na Mhe. Waziri anaweza kuniweka vizuri, nadhani hili jina halistahiki kuitwa kwetu, kwani kwa kadri ninavyofahamu kwamba kuna mikoa hapa majirani wenzetu wanalichukua jina hili kwamba ni lao wao. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro Mhe. Naibu Spika, ni mkoa wa viungo kuliko Zanzibar kwa kadri ninavyofahamu. Kwa maana hiyo ili Zanzibar irudi kwenye jina hili tunaloliita basi wizara hii ni lazima kwa karibu sana iwe pamoja na Wizara ya Kilimo na Maliasili kurejesha jina hili liwe stahiki kwa Zanzibar. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Zanzibar tunayo nafasi na fursa nzuri na hapa hapa niingize suala la viwanda. Kwa hivyo, viwanda vyetu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba Zanzibar haitomudu kuwa na viwanda vizito isipokuwa tutahitaji viwanda vidogo vidogo zaidi na viwanda vya kati. Kwa upande wa viwanda vidogo vidogo Mhe. Naibu Spiika, vitachukua hivi viungo lakini pia tutachukua mazao ya kilimo na mifugo pamoja na mazao ya baharini.

Mhe. Naibu Spika, hapa nazungumzia uhusiano wa viwanda na kilimo lakini taaluma hii pia kwa *technology* ya sasa, basi nataka Mhe. Waziri anielewe Mhe. Naibu Spika, kwamba mama yule kule Kajengwa aweze kusarifu mazao ya baharini aliyovua leo asubuhi na amalize *packing* pale pale na asafirishe kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa iliyotolewa Kajengwa Makunduchi. Micheweni, Tumbe, Msuka pamoja na Mtambwe ndicho ninachokizungumza hapa.

Katika hili Mhe. Naibu Spika, suala la nishati kwa sasa tutashindwa kufikia dhana tunayoizungumza. Kwa kweli nishati ni ghali mno Zanzibar na tunalipolisema kwamba kuna haja ya ndugu yangu Mufti Omar Yussuf Mzee Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa hivyo, tunaposema haja ya nishati kwamba tumiliki nishati kama Wazanzibari ni kwa sababu tuwawezeshe wananchi wetu kuitumia kwa bei nafuu na hii isionekane kuwa tunakufuru na wala hatukufuru, isipokuwa tunataka ‘maisha bora kwa kila Mtanzania’, yaani ni Mtanzania mpaka ambaye yuko kijijini. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, umeme leo Zanzibar si tu hata yule anayekwenda kununua pale LUKU au TUKUZA una kodi zaidi ya tatu. Lakini hata umeme wenyewe kwa jina lake bado ni ghali mno na kwa sababu ni ghali kwa kuwa na wenyewe tunaununua, yaani ni ununuzi wa biashara na anayeuza lazima apate faida. Sasa hata ukimfika mama au baba kijijini kazi imeshakuwa ngumu sana. Kwa kweli haja ya serikali kuutafuta umeme Zanzibar hili lisibezwe kwenye masuala ya upepo, jua na wala sisemi baharini naona kugumu zaidi, lakini hizi sehemu nyengine nadhani itaweza kutusaidia angalau kwa maeneo machache kama wataalamu walivyosema. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimalizie Wizara ya Kilimo na Maliasili iliyopita kulizungumzwa maghala ambapo yanafanyiwa ukarabati na niliuliza swali. Kwa hivyo, swali langu kwa Mhe. Waziri dhamira ya kuwa na maghala ya akiba ya chakula na fedha za serikali zinatengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi ama ukarabati maghala hayo ni kwamba yawe na hiyo akiba iliyokusudiwa ndani yake. Je, Mhe. Waziri tunayo akiba ya kiasi gani kwenye ghala hizo hadi sasa. Kutokana na hali hiyo wasi wasi wangu ni kwamba tunatumia fedha lakini hatufiki kwenye malengo yaliyokusudiwa. Malengo ni kwamba ghala iwe na akiba na wala tusisahau Mhe. Naibu Spika, ni karibuni tu tulikuwa na mtikisiko mkubwa sana wa chakula duniani Zanzibar, kamwe hatujafika uzalishaji hata wa nusu ya mahitaji na wala si vyema hata kidogo kukaa tukawa hatuna akiba ya chakula.

Mhe. Naibu Spika, jirani mpaka ashibe ndio akumbuke kwamba na mwenziwe kama hajala na wala hatatoa chakula chake akaja akakupa wewe. Kwa hiyo, Mhe. Waziri ndugu yangu katika mahangaiko na kutafuta kwake na timu ni nzuri sana aliyonayo, vijana bado wabichi wanao uwezo wa kuzunguka duniani. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, naomba sana haya ambayo nimeyataja na kuishauri wizara yake na Mwenyezi Mungu akujaalie uyaafikishe ndani ya miaka hii mitano tuliyoanza nayo tuiweke Zanzibar pale tunapotaka. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante na mimi nakushukuru kwa kujali muda. Sasa nafasi tunampa Mhe. Marina Joel Thomas baadaye Mhe. Ashura Sharif Ali na ajitayarishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na mchango wangu utakuwa katika maeneo matatu. Kwanza nitachangia kuhusu ukaguzi wa miradi ya wajasiriamali, pili Idara ya Maendeleo ya Viwanda na tatu Idara ya Mipango na Utafiti.

Kwanza kabisa naomba kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutayarisha hotuba hii ya bajeti pamoja na watendaji wake wote na kazi aliyoifanya ni nzuri. Katika kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 36, naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika.

Kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 36 unaeleza hivi:-

> “Jumla ya miradi 215 ya uzalishaji Unguja na Pemba ilikaguliwa kwa lengo la kubaini maendeleo yao na

changamoto zinazowakabili pamoja na kuwapa ushauri juu na namna ya kukabiliana na changamoto hizo".

Mhe. Naibu Spika, naomba niulize wizara baada ya kuangalia hizo changamoto pamoja na ushauri waliowapa, wizara kama wizara imepanga mikakati gani kwa sababu ukiangalia suala la viwanda ni suala ambalo vijana wengi wanapata ajira na wajasiriamali wetu wanajishughulisha. Ukiangalia suala la ajira katika nchi yetu ni tatizo. Wizara imetoa ushauri kwa wajisiriamali hawa lakini imeandaa mikakati gani zaidi ya kuanza kuwasaidia zaidi hawa wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia suala la Idara ya Maendeleo ya Viwanda. Katika ripoti ya Kamati ambayo aliwasilisha Mhe. Hija Hassan Hija alitoa takwimu hapa alisema katika diko la Maruhubi kunavuliwa tani 910 za dagaa bichi, akasema katika ripoti hiyo katika diko hilo limeweza kuwasaidia wananchi wetu ajira 1740.

Pato ambalo linapatikana kwa diko hilo la Maruhubi kwa mwezi walisema shilingi milioni 631. Kama ni hivyo basi nilikuwa naishauri wizara wawajengee mazingira mazuri wananchi hao ambao wameamua kujiajiri wenyewe, hasa tukizingatia sasa tatizo la ajira ni kuwa nchini. Diko hili kama tulivyoelezwa linaingiza fedha nyingi kwa mujibu wa takwimu alizotoa katika ripoti ya Kamati na vijana wengi wameajiriwa karibu 740, basi wizara iwajengee mazingira mazuri vijana wetu ili waendelee vizuri na miradi yao hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Idara ya Mipango na Utafiri. Hii ina jukumu la kufanya utafiti wa bidhaa mbali mbali na masoko. Wananchi wengi wamehamasika katika uzalishaji wa zao la mwani. Mwani unazalishwa mwingi kwa mujibu wa maelezo ya wananchi mbali mbali. Hapa nilikuwa naishauri wizara iongeze nguvu na umakini katika kufanya utafiti wa kina na uzalishaji wa bidhaa ya mwani ili kuona kwamba wana uhakika wa kupata soko la kuuzia bidhaa hiyo na hatimaye wananchi wetu wananufaika kutokana na shughuli zao wanazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, nende katika ukurasa wa 35 wamesema moja ya lengo la wizara limeanza kuimarisha zao la chumvi. Hivi sasa wanaendelea kufanya utafiti wa kitaalamu kwa zao hilo. Utafiti huo unajumuisha uzalishaji wa chumvi katika mashamba ya wakulima na usarifu wake katika kiwanda cha Wawi. Hapa nilikuwa naomba maelezo kwa sababu chumvi kuna baadhi ya wananchi na baadhi ya malalamiko wanasema kwamba baadhi ya chumvi zinakuwa hazina madini joto. Ukiangalia madini joto ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Ukikosa madini joto unaweza ukapata baada ya maradhi

kama goita na maradhi mengine. Kwa hivyo hapa nilikuwa naomba wizara ijiridhishe na kufanya uchunguzi zaidi ili kuona kwamba hizi chumvi zinazoingizwa zinazotengenezwa yamo hayo madini joto. Kama hazina ina maana wachukue jitihada za makusudi ili kuhakikisha chumvi hizo ambazo zinazalishwa zinayo mahitaji yao ya madini joto kwa sababu ni muhimu sana kwa binadamu.

Nende kwenye suala kama alilolisema mwenzangu Mhe. Ismail Jussa kuhusu ndimu ya unga. Ndimu ya unga kwa sasa ni matumizi makubwa sana hapa nchini na baadhi ya watu wengi wanatumia katika biashara hizi za mbatata za urojo na mambo mengine. Lakini ndimu ya unga hiyo hiyo ukiitumia katika matumizi ya kusafisha choo kwenye masinki, ukitia kwenye sinki la choo linakuwa kama karatasi kwa weupe. Sasa hilo ni sinki. Je, katika mwili wa binadamu inakuwaje. Nilikuwa naomba pia wizara ijiridhishe kwa uchunguzi, kama ndimu ya unga inasafisha sinki linakuwa jeupe ndani ya binadamu ina maana athari ikuwa kubwa zaidi. Kwa hivyo naomba pia ifanye uchunguzi wa zaidi ili kuhakikisha kwamba watumiaji hawapati athari katika matumizi yao ya ndimu ya unga.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu ni huo tu. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa uzima, akatuwezesha kukutana hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi kwa taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nianze pia na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake lakini pia niwapongeze watendaji wake kwa matayarisho ya kitabu chake hichi cha bajeti ambacho kinaonesha dhahiri kwamba walijipanga na wana nia ya kuweza kutekeleza yale ambayo wanayaombea. Yamekwenda kidogo na mambo yaliyotokea jana na juzi hadi kitabu kikapewa jina kitabu cheusi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli humu nimesoma katika hichi kitabu cha bajeti, nimeona mambo mengi na mazuri ambayo yakitekelezwa tunaweza tukafikia malengo. Nimeona nianze kuzungumzia kuhusu neno biashara.

Mhe. Naibu Spika, sote tunakumbuka kwamba Zanzibar kwenye historia inasomeka kwamba ni kitovu cha biashara, hakuna atakayebisha, historia ya kisiwa chetu kinajulikana kwingi duniani kwamba hichi ni kitovu cha biashara. Kwa kweli muda umekwenda siku zimesogea lakini waziri ana nia

njema na nzuri ya kuweza kuboresha hali hiyo na kuwafikisha wananchi pale wanapokusudia. Ningependa kusema yafuatayo:

Hayati Mzee Abeid Amani Karume alisema kwamba, "Mjenga nchi ni mwananchi". Mhe. Waziri katika hili ningependa kusema kuwazungumzia zaidi wafanyabiashara wa Darajani eneo la makontena. Mhe. Waziri eneo lile ndilo linaloonesha taswira ya mji wetu wa Zanzibar. Hakuna atakayepinga kuhusu hili mgeni yeyote anayetoka sehemu yoyote pale basi eneo lile ndio taswira inayoonesha mji wetu wa Zanzibar na shughuli zake zote na nyingi za kiuchumi hawa wananchi wetu watokao mashamba basi magari hufikia katika eleo lile. Ndipo panapoonesha shughuli mbali mbali za ki-mzunguko basi huonesha uhalisia wake wa shughuli za kibiashara.

Mhe. Waziri hapa nikwambie Wazanzibari wana sifa ya kupendena, wana sifa ya ukweli, wana sifa ya kukabili, wana sifa ya kujitolea, wana moyo wa kutoa sadaka. Nakwambia hili ni kuwa na maana kwamba Mhe. Waziri umefika wakati sasa ukae na wafanyabiashara wa Zanzibar wenye moyo na imani tuweze kuibadilisha taswira ya Darajani ilivyo ili ionekane hasa ni kitovu cha biashara kweli. Mhe. Waziri makontena matano yaliyokuwepo pale ambayo yanaleta ugomvi na mizozo mbali mbali hayajatosha. Kaa na wafanyabiashara ambao wana uwezo na wana moyo kama kaka yangu Bakhressa ambaye alijitolea yeye binafsi kujenga jengo kule bandarini na kuwastiri waajiria wetu ambao wanapata utulivu mkubwa.

Naamini kwamba wapo Wazanzibari wengi wenye moyo na wenye imani ya kujitolea kwa ajili ya kujenga katika eneo la Darajani maduka ya kisasa yanayoweza kuwa na uwezo mkubwa na kuweza kuajiri vijana wetu wengi. Nina imani kwamba kama pataboreshwa pahala pale pakajengwa majengo makubwa mazuri ya ghorofa tatu na nne, mimi naamini kwamba wapo Wazanzibari wenye uwezo huo, mtakaa nao na mmewapuuza kwa muda mrefu. Mfano ninakupeni majumba mengi yaliyokuwepo Dar-es-Salaam ni majumba ambayo yamejengwa na wafanyabiashara wa Zanzibar. Mji ule una taswira nyengine sasa unaonekana mzuri na unavutia. Kuna nini mpaka Wazanzibari hao wakatae kwao.

Mhe. Waziri nakuomba ukae na wafanyabiashara hao uzungumze nao, wakupe mbinu, utaratibu na nani anaweza. Umefika wakati sasa serikali yetu iweze kuwashirikisha wananchi wenyewe kwa ajili ya kuijenga Zanzibar yao. Naamini kwamba watakapolifanya hilo litajenga ajira kwa vijana wetu ambao ndio tatizo la taifa letu. Wale wanaotembea tembea huku na huku wakikosa kufanya shughuli zao, tukapigana vigongo, ule sio utamaduni wa Kizanzibari. Ni jambo ambalo linatuletea matatizo sisi wenyewe na kutuondolea mapenzi.

Wazanzibari si wagomvi, Wazanzibari ni wasikivu, nina imani kwamba wale vijana wanaohangaika na mikoba mikononi wale si wezi ni vijana wanaohitaji kuweza kupata sehemu ya kujitafutia rizki. Nina imani tukijenga kweli majengo mazuri, makubwa ambayo yatawawezesha kuingia juu na chini mzunguko wake, wale watakuwa wametulia katika maeneo yao hayo. Eneo la nje litakuwa zuri lina utulivu, soko limetuliwa na atakapokuja mgeni ataona hasa sasa nende sehemu fulani, liko duka fulani kwa utaratibu maalum.

Naamini tunaweza tukafika huko kama tutaweka nia hiyo. Naamini kuna Wazanzibari wazuri wenye imani kama ndugu yetu Said Bakhressa wanaweza wakalifanya hilo na tukafikia malengo yetu. Mhe. Waziri sasa nikikuachia hapo ni lazima vijana hao washughulikie ili tuone na ushirikiane hasa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, maana hapo kuna msongamano mkubwa. Wewe unawafanyabiashara lakini yeye yupo kwenye Manispaa ile ni Manipaa yake na mtunzaji wa Mji Mkongwe na yeye yupo hapa. Shirikianeni, umefika wakati wa sekta sote za serikali kukaa pamoja kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Lile ambalo linawezekana liweze kutekelezeka.

Mhe. Waziri sasa naona niguse kuhusu viwanda. Nimeona humu umegusa na kuzungumzia kwamba una nia nzuri kabisa ya kuviendeleza viwanda. Hili ni jambo zuri linatia moyo, litatoa tija na vijana wetu watapata ajira. Swali langu mimi ambalo linanipa mashaka kidogo ni kuona wawekezaji wetu wanapata mashaka na tabu kubwa kwa miundombinu yetu ya kukosa nishati. Nishati hii imekuwa ni tatizo sugu na mambo mengi ya viwanda yanahitaji nishati. Sijui Mhe. Waziri kwa kuwa humu umeeleza kwamba una nia hiyo ya kuboresha. Sijui una mpango gani wa kuona kwamba tunaweza tukapata nishati hiyo ili tukaweza kurejesha ile heshima yetu na historia yetu kuirejea ya kuwa na viwanda.

Si ajabu hili ulilolizungumza kwani naelewa kwamba tulikuwa na viwanda vingi kwenye historia yetu na viwanda hivyo vilikuwa zimeajiri watu wengi na watu wengi walitulia na uchumi wa nchi hii ulikuwa shwari, lakini leo vile vimepotea una nia ya kuvianzisha. Naomba utakapokuja hapa unieleze kidogo wewe una utararibu upi ili kuona kwamba tunafanikiwa hili. Tunaona kwamba nishati hii imekuwa ni ghali sana, tunainunua kwa gharama kubwa hasa kwenye uwekezaji ili hili liwe wewe una mpango gani madhubuti wa kuweza kuona tunafanikisha hivyo viwanda ili nia yako hii ikaweza kutekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, jengine nizungumzie kuhusu Kiwanda cha Sukari Mahonda. Mwaka jana wakati nikichangia nilikuwa na maswali mengi kuhusu Kiwanda cha Sukari Mahonda, jinsi ya mwekezaji aliyepewa ambaye

ameshindwa kukiendeleza. Ukanambia kwamba utanijibu kipo katika Kamati ya Wanasheria, jibu sikulipata. Kwa bahati katika kudadisi kwangu nilipenda kulielewa hili nikapata taarifa kwamba mwekezaji yule, sasa ameondoka kuna mwengine. Je, mkataba huu uliokuwepo baina ya yule aliyekuwepo mwanzo na huyu mpya nyinyi serikali mnaelewa hivyo.

Je, ana nia kweli ya kuendeleza kiwanda kile kwa sababu aliyekuwepo hadi hii leo hakuna mwananchi aliyepata faida ya uwekezaji ule kwenye ajira, wengine bado wanadai, watu wetu walitumwa kupanda miwa lakini hatimaye hawakulipwa. Raslimali zetu zilizokuwemo mle basi pia walifungua na kuchukua. Mhe. Waziri bado nina mashaka na mwekezaji huyo mwengine pamoja na hivyo unavyosema, lakini napenda unilitulize roho yangu, unambie kwamba huyu tuliyempa ana uwezo wa kukiendeleza kiwanda hicho.

Kwa masikitiko makubwa Mhe. Waziri nikwambie kwamba maeneo yaliyokuwa matupu ambayo amepewa mwekezaji kwa ajili ya kulima miwa mengine yalikuwa wazi kama ilivyokuwa mzozo uliotokea mwanzo. Wananchi waliwahi kulima pale na kwa bahati mbaya sana mpunga umekaribia kuvunwa mwekezaji kaamua kupeleka matrekta na mpunga ule umevurugwa ambao uko tayari kabisa kuvunwa. Kuna wananchi ambao wanapiga kelele na kulalamika juu ya zoezi lile.

Mhe. Naibu Spika, hebu Mhe. Waziri atwambie ni lini utakwenda kuwaona wakulima hao na ukae nao ili aone jinsi ya ile hasara. Wao waliamini kwamba mwekezaji wa mwanzo hakuwa na uwezo huo wa kijua na wa pili hana. Hawa ni wananchi wetu waliyopoteza nguvu zao, siku zote tunawapangia mipango ya dira za Mkuza I na Mkuza II ili tuweze kuwaongezea kipato na kuwapunguzia umaskini. Hali hiyo wamelima lakini kwa bahati mbaya sana hawakuweza kuvuna mwekezaji kawatuma watendaji wake wamevurugiwa mpunga wao wote. Je, wewe Mhe. Waziri unawambia nini wananchi wale, kwa kuwa nyuma yao walikuwa na hatia kubwa.

Baada ya kuyasema hayo sasa nije Shirika la *ZSTC*. Hapa hii karafuu inayotuongezea pato la taifa lakini lina hatua mbali mbali zinazofanyika ili liweze kufikia pahala liweze kuuzwa na kupatikana hizo fedha. Kuna wananchi wetu mbali mbali ambao wanahangaika kulivuna zao hilo na kwa bahati mbaya huwa wanaanguka. Watu hawa wapo wengi ambao bado hawajalipwa fedha zao tangu miaka ya nyuma.

Mhe. Waziri nikuombe sana hawa ndio wazalendo ambao pamoja na wao kupata maslahi lakini pia wanaongeza pato letu la taifa na kuona shughuli zetu zinakwenda katika ustari. Je, unanihakikishia vipi kwamba watapatiwa

na wao fedha zao. Wengine sasa hivi wamekuwa walemavu wapo katika hali nyengine.

Mhe. Waziri nakuomba sana hili ulione na uliangalie kwa moyo wa huruma. Sikuwa na nia ya kukuzuilia chochote kile ila nataka kupata ufafanuzi tu Mhe. Waziri kwa vile tangu ulivyoanza jana katika hotuba yako, ulianza na "*Au'dhubillahi, Minasheitwani Rajim*" Naamini kwamba shetani kakukimbia ukaanza na "*Bismillahi*", kwa hivyo ufunguzi wako ni mzuri, hivyo nasema kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ama nitakuwa ni mwizi wa fadhila kama sikukushukuru wewe kunipa nafasi hii ya kuchangia wizara muhimu, na bila ya biashara nchi hii isingekwenda. Waswahili wanasema kizuri kinajiuza kibaya kinajitembeza. Binadamu mara nyingi hasifiwi akiwa hai. Hukumbukwa na kumwagiwa sifa pale pumzi inapokatika. Mimi sitaki kuwa sawa na hawa, nataka kumsifu Mhe. Ahmed Mazrui akiwa na pumzi zake na mimi nikiwa na pumzi zangu.

Ni Waziri ambaye ameonesha mwanga mzuri wa nchi hii na mimi nataka kumpa nasaha kabisa Mhe. Naibu Spika, itakapofika wakati isije ikafika kama yaliyowakuta wizara iliyopita nyuma. Ukiona watendaji wako inafika wakati hamuelewani mimi nafikiri hata kujiuzulu kwa kulinda heshima yako. Mimi ninavyomkumbuka Mhe. Ahmed Mazrui katika utendaji wake sijasikia hata siku moja kugombana na mtu. Ni mtu msikivu, mfuatiliaji, hasubiri mafaili mpaka yafike juu ya meza, huyafuata kule yalipo. Watu wengi wamejenga imani sana na yeye hasa pale alipowakomboa wananchi wanyonge hasa wa kisiwani Pemba kwa kufuatilia kikamilifu zao la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nizungumzie kwa nia njema kabisa ya kuitetea Zanzibar na wananchi wake. Mhe. Naibu Spika, tupo hapa Wawakilishi kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar tumechaguliwa ili kuja kuwatetea wananchi wa visiwa hivi. Baada ya hapo nianze kuchangia bajeti ya Zanzibar nchi ambayo inavisiwa na uchumi wake unagegemea kodi na huduma kupitia sekta ya utalii na zao letu karafuu ambalo limepata mwanasiasa mahiri na muendeshaji.

Hata hivyo bado kuna umuhimu wa kuimarisha sekta na kukuza sekta za biashara, bahati mbaya hatuna mipango mizuri. Mfano kwa nini bandari ya Forodha Mchanga kwenye kufungwa. Katika kitabu hichi humu ndani kuna uongo mtupu, ni aibu na naweza kunukuu kama mambo mawili au matatu. Biashara ile ndio tunayoitegemea pale, leo tunaambiwa bandari imejengwa pale kukidhi mahitaji.Wallahi Ramadhani tunasema uongo humu ndani. Kuna

kitabu hichi cha sherehe za mapinduzi kinasema, juhudi zetu za kuimarisha bandari ya Malindi zinaendelea kuzaa matunda.

Idadi ya mizigo imeongezeka kutoka makontena 39,293 iliyopelekea mwaka 2011 hadi kufika mwaka 49,821 mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 27. Serikali imeshanunua mashine. Hapa ndipo ninapolia hapa. Serikali imeshanunua mashine mbali mbali za kunyanyua makontena zikiwemo *fork-lift* na *crane* maalum zenye uzito ambazo leo Wazanzibari kilio chao hichi. Hata Mhe. Waziri kazungumza hakuna *crane* inayofanya kazi, katika kama hichi imezungumzwa amani. Mimi nataka nikaoneshwe hiyo *crane* iko wapi iliyokuja katika kipindi hichi cha mwaka 2013. Si maneno yangu haya Mhe. Naibu Spika, maneno haya yamezungumzwa Uwanja wa Amani. Hatuwezi kwenda namna kama hii hapa tumekuja kujenga nchi, huduma hakuna mle ndani bandarini za vitendea kazi. Mimi nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa kulifuatilia hili na kuliona. Sisi tunategemea sekta ya magari, leo tunakuja eneo lile tunaambiwa bandari imetanguliwa ndani mle, vitendea kazi hakuna, pa kufungia meli hapana. Ikishakufunga meli moja tu pale hakuna, kitabu hichi, ripoti ya kudhibiti zoezi la uondoshaji wa bandari forodha mchanga, ndani humu uongo mtupu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba kitabu kinasema kwamba pamoja na hayo ukweli unabaki kuwa eneo la Forodha mchanga linakusudiwa kutumika kwa muda hadi itakapomalizika kujengwa gati kubwa ya Malindi. Tayari gati kubwa ya Malindi imeshajengwa na haikidhi. Leo hapa Mhe. Waziri anasema anataka kujenga bandari ya Mpiga Duri kuendeleza. Sasa mnakuja kudanganya mchana humu. Gati ya Malindi itamalizika kujengwa mwaka 2018 lakini hata baada ya kuanza kutumika gati kubwa ya Malindi meli hizo zitakuwa zimejengewa mazoea eneo la Forodha mchanga. Haieleweki, pale meli inakwenda masaa mawili tu, hii ni biashara.

Leo Wizara ya Fedha wamejitahidi sana mimi niwashukuru kwa kuweka kima kizuri cha ushuru wa magari, tofauti na wenzetu wa Bara. Wenzetu wa Tanzania Bara wanakuja kutumia soko hili kushusha magari yao kutoa hapa. Leo Mtanganyika anatoka Bara anakuja hapa anatumia *tax*, analala hoteli, anakula chakula, anapita madukani na kununua nguo na zawadi. Mhe. Mohammed Aboud naona hili suala mlifuatilie sana tusije tukatafuta mchawi, tukasema kwamba Zanzibar tumerogwa lakini tumejiroga wenyewe. Pale Forodha Mchanga meli inakaa masaa mawili au matatu kwa kupakia magari, ni magari mangapi kwa siku. Hatuwezi kwenda namna hii.

Wananchi hawathaminiwi kuliko Mji Mkongwe, Mji Mkongwe umevunja sheria ngapi humu, kuna mabanda bandarini kule yaliyovunjwa, tuna nia ya kuja kuwatetea wafanyabiashara wamekuwa wakiteseka, wakija wakitoa

ushuru Bara sisi tutaneemeka nini Zanzibar na pale hali wanakaa masaa mawili, saa moja na nusu, gari saba, kumi, mtu anapakia. Leo tunakosa biashara, Mhe. Waziri utakapokuja naomba unieleze na nasikitika sana kwa kuwa umeonewa na hukuifungua bandari ile, humu kuna sekta mbali mbali zimeshirikishwa, wewe hukushirikishwa. Mimi naamini usingekubali kutokana na utendaji wako.

Leo wanatunga sheria hakuna anayeshirikishwa kama Waziri wa Biashara ni sekta muhimu katika kitabu hiki kushirikishwa, anakuja kufunga bandari tunatafuta mapato tu, utayapata wapi mapato, tunatafuta mchawi, mchawi nani? Mapato hayawezi kuwa namna kama hii. Tuangalie Dubai, Wachina wameitwa, wamewekewa eneo lao wazi linaitwa *Dragon Market* Mheshimiwa nafikiri analijua jinsi wanavyoendesha biashara hiyo. Leo mzaliwa wa nchi hii anapigwa vita, mwekezaji atakuja kweli.

Mheshimiwa baada ya hapo nafikiri kwa utendaji wake watalifuatilia hili. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Bishara, Viwand na Masoko. Nianze kwa kumshukuru Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa muelekeo wao wa bajeti yao ambayo wamekuja kutuletea leo hapa.

Baada ya shukurani hizo nije moja kwa moja katika kitabu chetu cha bajeti ya mwaka 2012/13 ukurasa wa 3,1 naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

"Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya karafuu"

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya kitabu hichi Mhe. Waziri hapa ametuahidi kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya karafuu ili kuliendeleza zao la karafuu katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Lakini kwa bahati mbaya katika kitabu cha bajeti yetu mpya hatukuona maendeleo ya mfujo ule wala hatuna taarifa juu ya mfuko ule kwamba umeanzishwa au una matatizo gani. Ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa sababu mfuko huu aliahidi kuanzisha katika kikao cha mwezi wa Septemba 2012, atakapokuja hapa atwambie mfuko ule umefikia hatua gani na nini kinaendelea katika suala hilo la kuanzisha huo mfuko na kama tumekwama ni kwa sababu zipi.

Nikiondoka hapo nakuja katika ukurasa wa 59 kitabu hicho hicho cha mwaka jana katika suala la *MTC*. Mhe. Naibu Spika, katika kitabu kilichopita tulipata maelekezo ya namna gani serikali ilivyokuwa imejipanga kupitia katika wizara hii juu ya kufikia muafaka katika suala zima la *MTC*. Lakini kitabu

chetu cha mara hii kilichokuja tumepata maelekezo kwamba suala hili limepelekwa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufikia mustakbali wa suala hili.

Tungemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleweshe ni lini suala hili litakuwa limekwisha ili kuwaondolea uzia wale watu ambao wanafanya kazi katika shirika hili waweze kujitambua. Kwa sababu hawawezi kuendeleza biashara, hawawezi kuacha biashara wala hawajijui nini hasa wanafanya tungemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kutueleweshe juu ya suala hili.

Suala jengine ningelimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni kwa sababu zipi Baraza lake hili tukufu halipati taarifa muhimu kuhusiana na Baraza la Biashara la Zanzibar. Chombo hiki Mhe. Naibu Spika, ni chombo muhimu na ni chombo ambacho kinaweza kutatua matatizo mengi yanayowakabili Wazanzibari katika kadhia mbali mbali ambazo tunaendelea nazo. Sasa ni sababu zipi ambazo wajumbe hawapati taarifa za haya maendeleo ya *ZBC* katika harakati zetu za utendaji wa siku hadi siku.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka kumtanabaisha tu Mhe. Waziri kwamba yeye ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko lakini ni mfanyabiashara wa kutambulika ndani ya visiwa vya Zanzibar na nje ya Zanzibar na bahati nzuri zaidi Mhe. Waziri aliwahi kutokea Taasisi ya Umoja wa Wafanyabiashara Zanzibar na kuweza kufikia nafasi ya kuwa yeye ni Rais wa Wafanyabiashara wa Zanzibar. Lakini tokea tumekabidhiwa na tumemkabidhi Wizara hii bado tatizo sugu na tatizo la uhaulishaji wa mizigo baina ya Tanzania Bara na Visiwa vya Zanzibar vingali vinaendelea. Wafanyabiashara wa Zanzibar wana matumaini makubwa sana na kuwa ndugu yetu Ahmed Nassor Mazrui kuwa Waziri katika Wizara hii, na kuona kwamba tatizo hili, pumu imepata mkohozi. Lakini hadi leo hii bado tatizo hili hatujafikia muafaka na ukitilia maanani zaidi kwamba matatizo ambayo yanayakabili uhaulishaji wa mizigo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara si ya kisheria. Ni matatizo ambayo yanasababishwa na ndugu zetu wa *TRA*.

Sasa nataka kufahamu ni juhudi gani binafsi ambazo Mhe. Waziri amezichukua kuhakikisha kwamba kadhia hii inamalizika kabisa katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Vile vile anipe ahadi yake kabla hajaondoka ni nini atawaahidi Wazanzibari katika kuondosha kadhia ya uhaulishaji wa mizigo baina ya visiwa vya Zanzibar na Bara.

Jengine nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anielezee ni kwa kiasi gani serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kupata hasara katika uingizwaji kwa mchele kwa wananchi wa Zanzibar, kwa sababu kwa mujibu wa sheria ya *East African Community* kuna makubaliano ya kuwa tufuate

rates moja, lakini Zanzibar tuna utaratibu wetu. Sasa ningelipenda kufahamu ni kiasi gani serikali inaendelea kupata hasara ili kuwasaidia Wazanzibari waweze kuendelea kuhimili kuinua zao hili kubwa na chakula muhimu katika nchi yetu.

Jengine na la mwisho Mhe. Naibu Spika, ninaipongeza sana Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa jitihada zake inazofanya kuwatafutia soko wajasiriamali ambao tunao Zanzibar. Lakini kuna tatizo ambalo linajitokeza, watu hawa wanapokwenda na bidhaa zao wanapata masoko katika maeneo ambayo yanakwenda kuuza biashara hizi. Sasa lakini uwezo wa kuweza kukidhi yale masoko au yale mahitaji ambayo yanahitajika kwa wale ambao wamewapa *order* hayawezi kutimizwa kutokana na uwezo wao mdogo ambao wanakabiliana nao.

Sasa ningelipenda kufahamu Wizara yake inajipanga vipi kuhakikisha kwamba inawasaidia hawa wajasiriamali ambao wanapata soko kubwa la kuuza bidhaa zao lakini uwezo wao ni mdogo.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 90 kumi nabakisha baada ya kwisha kupewa maelekezo yatakayoniridhisha.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii sote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uwezo na pumzi katika hili Baraza lako kuendelea kuwepo hapa sisi kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, kwanza ninashukuru kwamba hii Wizara imetugusa sote lakini mimi ni fani yangu kama mfanyabiashara na ninashukuru kwa heshima na taadhima kwa kupata nafasi hii.

Mhe. Spika, nataka kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na uongozi wake mzima kwa hekma, busara na usikivu na shughuli zote alizokuwa anazifanya. Lakini vile vile Mhe. Nassor kaka yangu, mwenzangu, ndugu yangu na tunatoka mbali. Sasa ninachotaka kumwambia tu Mhe. Nassor umekuwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwa bahati Mwenyezi Mungu kakujaalia uko bondeni huko Waziri na mimi nilikuwa mfanyabiashara niko *backbencher*, matumaini ya Wazanzibari hasa wafanyabiashara kwamba tutawatumia kwa maslahi ya wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, nataka kumwambia tu ndugu yangu Mhe. Nassor uongozi ni dhamana na uongozi ni kupita, hapa nilipo mimi na alipo yeye kuna siku

sote tutaondoka. Haya tuliyoyapanda ma-*PRADO*, haya yote yatatutoka siku moja lakini tuweke alama katika nchi hii. Sasa Mhe. Waziri ninamwambia hivyo ninampa ushauri. Mimi naunga mkono bajeti yake tena asilimia 110 sio mia tu lakini nataka kumpa ushauri kwa maslahi ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, nataka kumkumbusha Mhe. Waziri kwamba tulihangaika sana tokeoa huko tulianza na biashara zetu za bafta, sabuni, sote tunatoka huko tulikotoka kwa wananchi.

Sasa Mhe. Waziri nataka kumwambia suala la soko la biashara. Mhe. Naibu Spika, kuna biashara *competition* haimo ndani ya muungano na historia hata hizo meli wakati huo zote zikija Zanzibar zikifanya biashara na maji zikichukua kutoka Zanzibar. Kuna suala hili la vitendea kazi ambapo wananchi wanaotumia magari yao ya michanga na kokoto na kuna biashara nyingi, leo wenzetu Bara, tukenda nje tukitaka kununua vifaa hivi wanatwambia kuna *agent*. Sasa tumejaribu kuwaelimisha sana Tanzania maana yake ni Zanzibar ndio tukaita Tanzania.

Sasa hili Mhe. Waziri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kula hasara katika kila sehemu kwa sababu inabidi vifaa hivi huwezi kupata kwa sababu wenzetu kule wameweka wao *labour* yao. Lakini masuala ya biashara hayamo kwenye muungano na Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika, hili nililizungumza mwaka jana. Sasa nataka nimwambie Mhe. Waziri wa Biashara, haya matairi tunayoyazungumza hapa T38 yale ma-*PRADO* yetu tuliyoyaweka nje hayatumiki yale, haya yanatumika kwa wananchi walio wengi, wenye kokoto magari, gari za mchanga. Sasa tuwasaidie kuwapunguzia makali ya bei kwa sababu vifaa hivi inabidi kama unavitoa China, unavitoa Dubai, Dubai unavileta Zanzibar.

Mimi ninafikiri Mhe. Waziri Mhe. Naibu Spika, katika hili awe wazi na kuelezea na kutoa msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukaa na Waziri wake wa Biashara na mabalozi kwamba bwana kuna masuala mengine ni ya Zanzibar hayamo. Hilo la kwanza.

Lakini Mhe. Naibu Spika, hili suala la Afrika Mashariki na Kati soko la pamoja na yeye sasa ni mjumbe wa Baraza la Mapinduzi, kuna mambo mengi ndani ya Baraza la Mapinduzi yamepitishwa, mimi nina ushahidi maana nimekuja huku toka ninapozungumza mpaka leo alhamdulillahi ninamshukuru Mwenyezi Mungu vitu vyote na nini hata hayo niliyoyaelezea nimeshaelezea miaka 20, lakini ninakuja kuweka rekodi tu katika hii miaka 20 haya yote ninayoyazungumza nimeshayaelezea Afrika Mashariki na ya Kati. Mheshimiwa awamu ya tano Rais wa Jamhuri ya Muungano Rais Mkapa kwa ushahidi walituletea dokezo Zanzibar kuhusu Afrika Mashariki na ya Kati Zanzibar mnasemaje?

Sisi Zanzibar tukajibu kwa maandishi, awamu ya tano Rais aliyekuwepo madarakani akatia saini, tukawapelekea wenzetu jamani kwa kuwa Afrika Mashariki na biashara haimo ndani ya muungano, michezo, kilimo mambo mengi tuachie Zanzibar tuingie kama Zanzibar, kule kuna biashara wewe hohe hahe. Mimi tukapeleka. Matokeo yake Mhe. Naibu Spika, vitu hivi hatukuweza kwenda na nataka nimwambie Mhe. Waziri kama hajasimamia hivi hazitoweza kutekelezeka. Wenzetu Kenya wameingia kama Kenya, Uganda wameingia kama Uganda, Tanzania hawawezi kuingia bila ya Zanzibar. Sasa ilikuwa lazima tukae kwa pamoja. Pale Afrika Mashariki anakwenda Waziri wa Tanganyika au Tanzania Bara, sasa huku Zanzibar anatuwakilisha nani?

Sasa Mhe. Naibu Spika, nataka nielezee haya mambo kwa kupendana na kwa kushirikiana. Sasa nataka Waziri wa Biashara kwa sababu alikuwa mfanyabiashara na haya mambo yote anayajua na anayafahamu. Kwa hivyo tuwe wazi katika hili katika kusaidia na kusaidia viongozi, haya mambo yameanza siku nyingi. Sasa katika Afrika ya Mashariki na Kati tunakwenda kwenye soko moja, soko moja kwa kitu gani. Sasa ninafikiri lazima tufikie mipaka ya watu kukaa kwa pamoja kujadiliana na kuzungumza kwa pamoja.

Suala la *COMESA* Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri tulikuwa pamoja yeye alikuwa *chamber*, Zanzibar tuliingia pale kama tunatafuta uchumi wetu, Bara walipoona choyo, maandishi yapo, *documents* zipo Mheshimiwa wakatwambia aah! hamuwezi kuingia, wao hawakuingia na sisi hatukuingia kukawa na kazi kubwa. Mhe. Nassor Waziri wa Biashara akiwa *chamber* anaelewa yote hayo. Sasa mimi ninafikiri Mhe. Naibu Spika, nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba *we are all in transit* kama haya mambo hatukuwa wakweli sisi na yeye mfanyabiashara kayaona masuala ya biashara tutaendelea kuwa na matatizo kama haya, kwa sababu katika masuala ya biashara hivi karibuni *TRA* wakikuta tu vyombo viko njiani wameshavikamata wanasema magendo. Sasa hivi vyombo vinakwenda kwenye taratibu vikifika bandari ya Dar es Salaam *charge* au ziangalie lakini unakwenda kumkamata mtu kati kati ya bahari unamwambia magendo hajafika huko mashariki, hawajafika magharibi.

Mimi ninafikiri Mhe. Waziri tuko tayari kumsaidia aweze kulisaidia hili. Mhe. Naibu Spika, nataka kumwambia Mhe. Waziri, soko la biashara ni soko huru kwa Bara na Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, naelewa ndugu yangu Sheikh Nassor ninamkumbusha ninampa ushauri tulipata hapa ndugu yetu kutoka Dubai Mzee Luta ambaye mtoto wake leo ndio Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ya Serikali ya Abu Dhabi. *Zanzibar Air Line* imo kwenye vitabu Luta huyo alikuja Zanzibar kwa mara ya kwanza alilipenda jina la Zanzibar tu alhamdulillahi kataka kuanzisha kwa ndege tatu rekodi ipo BLM, iko

serikalini. Mimi ndiye niliyempokea nina uchungu na nchi, nilivyompokea nikamwambia bwana Zanzibar, nikamwambia Zanzibar hohe hahe, suala la dola moja kuchangia hatuna kwa maandishi tena, alifikia Ikulu Boznia hapo. Akasema nitakupeni Wazanzibari asilimia 35% *as fare*, nitaleta 767 mbili, nitaleta 737 moja ya kwenda sehemu zote. Dr Hikman yule Mwenyezi Mungu ampe uhai na uzima na afya njema, Mkurugenzi aliyepewa *ZIPA* pale tukenda Dar es Salaam, maana sisi kila jambo tunachotaka tukapige magoti kule chochote kile, lakini wenzetu wanapotaka kuamua mambo wao hawataki kibali kabisa na muungano huu ni wa serikali mbili. Ndio maana tukaita Serikali ya Tanzania; nchi mbili huru. Ukenda Dar es Salaam Mhe. Naibu Spika, rekodi ipo, serikalini ipo, wanatuambia nyinyi Zanzibar mnataka kuua *Air Tanzania* kwa nini mnataka kuanzisha shirika la ndege, wallahi hayo ndio majibu tukakataliwa. Kitabu hiki zaidi ya miaka 20 nimekizungumza. Yule mzee mimi nikaona haya na pale alipofikia nikaona tabu, wenzetu hawa wa Bara Idara ya Anga na Wizara ya Miunduombinu leo umewakaribisha *first jet* ambao ni wawekezaji kutoka Uingereza wamepewa kibali ya kuruka sehemu yote wanayoitaka. Sisi Wazanzibari tumeungana udugu, kwa mapenzi, kwa kuaminiana, wakatuwekea vikwazo. Wenzetu ile pale *first jet* kampuni inatoka Uingereza kule.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hivi vielelezo vyote vipo na serikali vipo. Sasa nataka kumwamba Waziri wa Biashara awe muwazi na jambo hili bora aombe apumzishwe lakini ana dhamana kwa Mungu, yeye ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, tukifika saa 6 hapa sote tunakimbialia kusali pale kwa sababu tunataka thawabu zetu. Leo tunakimbilia kufunga kwa sababu tunataka thawabu. Lakini kuna mambo lazima tuwatumikie wananchi tumewafanyia nini wananchi wetu katika uongozi wetu. Mimi siilaumu hii awamu ya saba Dr. Shein Rais wetu mpenzi wetu, haya mambo kayakuta sasa kazi yetu ni sisi kusaidiana.

Kwa hivyo nataka kumwambia Mhe. Waziri tusipokaa na kuona kwamba hali hii namna gani ya kukaa, nasema Mhe. Waziri kwa sababu ni fani yake biashara haya mambo yote anaelewa. Leo kawa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mungu amzidishie, yupo yuko chini akitoka anatafuta *PRADO* yake. Lakini tulipotoka kule tulikuwa na mafuta yetu na baiskeli zetu lakini leo Mwenyezi Mungu katufikisha hapa. Ninachotaka kumshauri Mhe. Waziri ninamuheshimu sana tena mwenzangu kwamba maslahi ya nchi tuweke mbele, maslahi ya kuwatumikia wananchi tuweke mbele, tumo humu ndani tunatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumo humu ndani chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hata hii ilani aliyoisoma Mhe. Waziri kaka yangu Mhe. Nassor Mzrui ni ilani ya Chama cha Mapinduzi, hakuitoa yeye. Sasa mimi ninafikiri tufike Mhe. Waziri awe muwazi na azungumze kutokana na hali ilivyo, tuko hohe hahe.

Lakini la mwisho nataka kumshauri Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Miundombinu kama kweli tunataka kuwaondolea umaskini wakulima na hawa wananchi wetu vijijini, kama hatukuwa na sera maalum ya kutengeneza barabara zetu za ndani za miundombinu bado umaskini kwa wakulima na wana vijiji wataendelea kuteseka bila ya kuona jinsi gani. Mimi niko tayari kushirikiana na Waziri Mhe. Nassor hizi barabara zetu za ndani kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, tatizo si itakuwa *diesel*, nitakaa naye tutakwenda pamoja kote huko. Tutakwenda Marekani, Uingereza, Abu Dhabi, Muscat, Denmark kusaidia wananchi kwa mambo ya mafuta tu hayo lakini vile vya ndani.

Kwa hivyo ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri vile vile kuna ahadi niliiotoa lakini kutokana na sababu ambazo za msingi nikakubaliana nao, mimi niliitoa mwaka jana ninamshukuru na ninashukuru Mwenyezi nimelivua kwa Mwenyezi Mungu amenihukumu nia yangu, na wao wakanielewa na mimi nikawaelewa taratibu. Lakini vile vile nataka nimshauri Mhe. Waziri wenzetu hawa wa marikiti Mhe. Naibu Spika, nipo hapa kwa maslahi ya wa marikiti hawa wakipewa mikopo midogo midogo tu wanarejesha. Mhe. Naibu Spika, mimi natamka wazi kawaulizeni wale marikiti wauza samaki wale wanaouza mboga mboga, wale mimi nimeanza kuwapa mikopo mimi kama *Raza Hassan and Sons*, huyu laki mbili, huyu laki tatu, huyu laki nne kwa wauza mboga, ndimu kwenye soko la Mwanakwerekwe wananisikia kwenye TV wote na nikaambia hivi, ninakupeni mkopo huu nikitangulia mimi mbele ya haki mtailipa familia yangu ukitangulia wewe mbele ya haki ninakusamehe. Maana wewe unauza samaki, mimi nikadai familia yangu hohe hahe, ninakusamehe lakini nikitangulia mimi nimeanza kusema mimi kutangulia sio yeye.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari ni wasikivu, hawana shida hata wakulima hawana kazi ya kuomba kuomba tukiwasaidia tutaweza kufikisha na kuwasaidia pahala pakubwa. Kwa kumalizia mimi naitakia kheri Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na narejea tena naiunga mkono tena asilimia 110 katika Wizara hii. Matumaini yangu kwa Wawakilishi ninawaomba kwa kumjua Mhe. Nassor Mazrui naomba buti zisiwe nyingi tupitishe bajeti hii tumalize hasa kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Raza kabla sijamwita Mhe. Hassan pana tangazo limeletwa na Sheikh Mussa Ali Hassan Mwakilishi wa Jimbo la Koani anatualika sote Waheshimiwa futari itakayofanyika katika Skuli ya Koani saa 11, gari zitakuwepo Barazani hapa wanaoshiriki kwenda aje, gari ipo watapelekwa na kurudishwa. Kwa hivyo Sheikh anakuombeni sana Sheikh Mussa Ali Hassan wa Jimbo la Koani mshirikiane naye.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Dakika tano ulizonipa nitazitumia vizuri nitamalizia kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kabla yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu na kusimama mbele ya Baraza lako tukufu. Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kitabu chao kizuri kilichopambika na chenye matumaini makubwa. Inshaalla Mwenyezi Mungu ampe uwezo mkubwa afanikishe haya aliyokusudia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu kama Zanzibar kama ilivyoelezwa ni kitovu cha biashara, kama tutakuwa wakweli na haya tunayoyazungumza basi wananchi wetu wataondokana na umaskini watapunguza umaskini, tukiwa wakweli. La kama tutazungumza kwenye vitabu hivi na sisi tuzungumze hapa tuondoke zetu hakuna ukweli ndani yake siku hadi siku tutasikia bado tuko maskini.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika ukurasa wa 18 imeelezwa kuwapo na mpango wa kufanya Zanzibar eneo tengefu la uchumi na kuweka mikakati kwa pamoja na kutangaza kwa lengo la kuwavutia wawekezaji. Hili ni jambo zuri kama litafanywa kama lilivyokusudiwa ni jambo zuri sana na tuombe Mwenyezi Mungu amsaidie Mhe. Waziri wetu afanikishe jambo hilo. Lakini kakusudia mipango hii basi kunakuwa na mipango mizuri, kama tumekusudia kufanya hivyo mimi nasema basi kuwepo kwa bandari huru itasaidia kufanikisha jambo letu hili. Itakumbukwa utawala wa Mhe. Rais Mstaafu Dr. Salmin Amour alijaribu kufanya bandari huru hapa na tuliona maendeleo makubwa, wafanyabiashara walikuwa hawatoki. Kulikuwa na meli ya Commoro ilikuwa inakuja siku hadi siku ndani ya wiki na meli ile ilikuwa na wafanyabiashara wengi wakichukua mali Zanzibar kupeleka kwao na ndugu zetu wa-Tanganyika Mikoa mbali mbali walikuwa wanafikia hapa.

Sasa kama hilo tutalifanya tutafanikisha na tulione kabisa kabisa. Kwa hivyo wale wanaokuja kuchukua biashara kutoka Zanzibar wanaofanya biashara ni wananchi wetu wanapata wateja mbali mbali ikiwa litatekelezwa hilo, basi mambo yetu yatakuwa mazuri. Lakini kwamba haitoshi kufikia huko lazima kuwe na miundombinu ya uhakika ya mawasiliano na uchukuzi. Tukiwa na miundombinu ya uhakika ya mawasiliano na uchukuzi basi watu watembee na Zanzibar siku hadi siku wateja wafanya biashara wataingia katika nchi ya Zanzibar. Meli zikifika pale uchukuzi ukiwa mzuri watu wanapenda kule

kunakuwa hakuna muda mkubwa wa kuweka meli, kupakua mizigo basi itapendwa Zanzibar.

Lakini vile vile inakuwa haitoshi kuwepo na usafiri wa uhakika wa baharini, ardhini pamoja na usafiri wa anga huu utatuletea tija sana. Mhe. Mjumbe aliyekaa kitako sasa kazungumza kwamba barabara zetu zikiwa nzuri basi hata uzalishaji unakuwa mzuri, kwa sababu mtu ana uhakika anakwenda sehemu kufanya kazi muda fulani anarudi, ana uhakika basi usafiri ukiwa mzuri wa ardhini, baharini na usafiri wa anga watu watapenda kitu kama kipo Zanzibar watu watakifuatilia hawana tabu yoyote anajua kwamba usafiri wa uhakika muda wote anakwenda anarudi.

Lakini haitoshi Mhe. Naibu Spika, ulinzi na usalama wa watu na mali zao ni jambo ambalo litakuwa ni kivutio kikubwa lakini angalieni leo muuza dagaa anapigwa katika vichochoro kwa kuuza dagaa. Ulinzi unakuwa si mzuri lakini hawa wakilindwa basi watakuwa na moyo wa kuja Zanzibar kama ni mahali pa usalama na amani. Jambo hilo tukiwa nalo tutafarijika kweli kweli na Zanzibar itapendeza kuliko tulikotoka. Lakini vile vile tuwe na mpango wa kutanua masoko yetu ya ndani na ya nje, masoko yetu ya ndani haya tukiyaboresha yakiwa mazuri kutafuta masoko ya ndani na nje basi bidhaa zetu zitauzika vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikenda katika ukurasa wa 27 hapa imeelezwa juhudi za serikali katika kutafuta masoko na bidhaa zinazozalishwa Zanzibar jambo zuri sana, lakini tukiangalia tulikotoka Zanzibar hii kulikuwa na mambo mengi tu mazuri yaliyohusiana na biashara, ukiangalia kwa muhtasari mambo yote yale yamekufa. Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Waziri ajaribu kufufua mambo haya, akifungua mambo haya basi inshaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nchi yetu itakuwa na neema kubwa. Tulikuwa na zao la mbata hapa, hili lilishamiri sana Zanzibar na bidhaa ya mafuta ya nazi ilikuwepo iangaliwe biashara hiyo, leo ipo tena hapa ni matatizo. Basi mambo haya yakifufuliwa biashara zinakuwa siku hadi siku.

Hapa palikuwa na uzalishaji wa pilipili hoho, kungumanga, popoo hata mafuta ya chikichi yalikuwepo lakini sasa hivi yote yale yamepotea. Tukitunza mambo yetu haya tutafarijika vya kutosha. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na viwanda vya masufuria tena yaliyo bora hayapo, tulikuwa na kiwanda cha maziwa, maziwa yalikuwa mazuri kabisa tukisafirisha mpaka Dar es Salaam mambo yote hayapo. Tulikuwa na kiwanda cha viatu vya ngozi, mwendo mtu alikuwa anapiga kanzu yetu vizuri kama mheshimiwa alivyopendeza na bakora yake anatembea vizuri lakini yale yote hayapo tena. Tunaomba Mhe. Waziri ujitahidi ufufue mambo haya ndio mambo yetu ya asili na mazuri yaliyopendeza katika mji wetu.

Lakini ni vyema katika kufikia huko kujengwe soko maalum ambayo *super market* ya *spices* zetu hizi, mtu akitoka akenda kule vitu vimepangwa vizuri katika *super market* ile ataona ubora wa hali ya juu. Lakini angalieni leo pale Darajani vitu vinapangwa chini ovyo ovyo haipendezi, lakini kama tungefanya hivyo tunaona tunatembea nchi za wenzetu jinsi wanavyofanya mambo yao mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia tu niendelee kidogo katika ukurasa wa 34 kifungu cha 70 pale, imeelezwa mambo muhimu sana ambayo iwapo yatashughulikiwa ipasavyo hapana shaka Zanzibar inaweza kuibuka kidedea. Imeelezwa pale kuna usarifu wa dagaa, hili likishashughukiwa vizuri kutakuwa na mapato yanaingia lakini mimi nasema kiini macho nilizungumza katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama sheria ile ni nzito lakini Mhe. Mazrui anazungumzia usarifu wa dagaa, ajue kama linavuliwa na nyavu ndogo ndogo na nyavu ndogo ndogo zinapigwa marufuku. Jee, ukizuia nyavu ndogo ndogo dagaa hili tutalipata kulisarifu. Jibu mimi nasema kuwa hapana. Sasa kumbe tumeona kwamba umakini wa kupata hili dagaa kulisarifu. Mhe. Waziri jitahidi lakini na Waziri wa Mifugo na Uvuvi ifahamu kama dagaa linavuliwa kwa nyavu ndogo ndogo na hata ukiangalia walaji wetu wengi ni wa dagaa kwa sababu wananchi wetu maskini. Nasikia pale likinadiwa tonge kwa tonge la kuosha watu wananadi pale pale. Kwa hivyo idhibitiwe sana kuimarisha uvuvi, ufugaji na kilimo basi shughuli zetu zitakwenda vizuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu muda umetukwaza na leo ni siku ya Ijumaa naomba niishie hapo na mimi naunga mkono hoja hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kojani naunga mkono asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo hii tukaweza kufika Ramadhan ya 24 na tuendelee kumuomba kwamba atujaalie tuweze kukamilisha Ramadhani hii funga zetu atukubalie.

Mhe. Naibu Spika, nikushukukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba yetu hii ya Wizara ya Biashara kwa mwaka huu wa fedha 2013/14. Shukurani nyingi Mhe. Naibu Spika, nazipeleka kwa Wajumbe wote wa Baraza lako hili bila ya kuwasahau kabisa Kamati ile ya Fedha, Biashara na Kilimo na nimshukuru sana aliyewasilisha ripoti ile kwa niaba ya Kamati Mhe. Hija Hassan Hija. Nawashukuru wote waliochangia Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wote Waheshimiwa walikuwa 19 na watatu walichangia kwa maandishi. Mhe. Naibu Spika, nawashukuru wote na nasema kwamba kwa kuwa wametuunga mkono tunawashukuru sana na kwa wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ni kutokana na ufinyu wa muda,

lakini naamini pia ni kutokana na ubora wa hotuba yetu ambayo tumeiwasilisha hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla niseme kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, tumepokea hoja, masuala na mapendekezo ya Waheshimiwa wote kuhusu utekelezaji wa bajeti hii na ninaomba basi niweze kufanya majumuisho kwa pamoja kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wako wakati wakichangia kulikuwa na hoja ya uhaba wa wataalamu katika Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko, tunakubaliana nao katika hoja hii na zaidi kwa kuwa kumekuwa na taasisi ambazo imebidi tuziongeze kwenye Wizara yetu ili iweze kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake. Lakini katika kulifanyia kazi hili Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukiwasiliana na Wizara husika ya Utumishi ili kusaidia katika uajiri wa wataalamu na kama alivyosoma Mhe. Waziri kwenye bajeti yetu ni kwamba tayari tumeshaajiri wataalmu wanne, wawili katika sekta ya vipimo lakini pia wafanyakazi sita katika sekta ya viwanda, mahitaji ni wanne lakini mpaka sasa kwenye sekta ya vipimo tumeweza kupatiwa nafasi mbili.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limejitokeza katika wachangiaji wakati wakichangia Waheshimiwa ni kuhusu suala zima la uzalishaji wa chumvi. Nataka niwakumbushe Waheshimiwa kwamba suala hili tayari tumeshakuwa tukilijibu katika kipindi cha maswali na majibu ya Baraza la Wawakilishi lakini nawakikishia kwamba tumelifanyia kazi kwa kiasi kikubwa, tumefanya ziara kutembelea hawa wananchi wanaozalisha chumvi na zaidi katika kile kiwanda kilichopo pale Wawi. Katika kulifanyia utafiti suala hili Wizara imewasiliana na Shirika la *TIRDO* Tanzania Bara ili waweze kusaidia basi kuongeza au kuhuisha chumvi ambayo itakuwa inazalishwa. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa ni kwamba ile chumvi inayozalishwa haikauki vile ipasavyo inabakia inakuwa ina maji maji, mashine zile zinazokaushia zina matatizo au haziendani na chumvi inayozalishwa. Kwa hivyo kwa kushirikiana na *TIRDO* kutoka Tanzania Bara, wizara inalifanyia utafiti suala hili na inshallah tukipata matokeo yake Waheshimiwa wataelezwa.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa masuala mengine yanayojitokeza ni suala zima la upandaji wa bei wa vyakula. Tatizo hili naomba tukubaliane na Waheshimiwa kwamba kwa kiasi kikubwa Wizara tumeweza kulifanyia kazi na kwa mashirikiano makubwa sana na wafanyabiashara wanaleta bidhaa hizi za vyakula wamekubali tumekuwa tunakaa nao kwa utaratibu maalumu ili

kukubaliana juu ya bei hizi za vyakula na zaidi bidhaa za mchele, sukari na unga wa ngano.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana wafanyabiashara kupitia Baraza hili tukufu kwamba utaratibu huu tunaendelea nao kwa uzuri na mpaka sasa hakuna tatizo lolote.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limejitokeza hapa wakati wanachangia hotuba hii Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukuku ni pamoja na kuongeza kasi ya ukaguzi wa bidhaa hizi za vyakula, kwa sababu katika jamii yoyote, naomba tukubaliane kwamba wafanyabiashara wengi wao ni waaminifu lakini wadanganyifu wachache hawakosekani. Kwa hivyo namna wanavyozijua wenyewe hupenyeza-penyeza hizi bidhaa ambazo zimeshapitwa na wakati au labda zinakaribia kumaliza muda wake wa ubora. Sasa niwashukuru sana wananchi walio wengi tunashirikiana nao vizuri kwenye Wizara yetu wakipata bidhaa kama hizo hutufikishia pale Wizarani na hutupa taarifa kamili wamenunua wapi na kwa mfanyabiashara gani na kwa mashirikiano na wataalamu kutoka Wizara ya Biashara, basi tunafuatilia suala hilo kwa umakini na naomba niwaambie wafanyabiashara kwamba wanatoa mashirikiano na taasisi zetu hizi, lakini tunaomba wawe waaminifu basi ili tusiweze kuwauzia wananchi wetu bidhaa ambazo zimepitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, lakini pamoja na hayo yote tukubali kwamba iko haja ya kuongeza kasi katika kulifanyia kazi hili kwa sababu wafanyabiashara wanatumia ujanja wa aina nyingi kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa wakati wanachangia wametukumbusha hapa kwamba huwa wanabadilisha mpaka vile vifurushi ambavyo vinakuja na bidhaa na zaidi sana ni mchele na unga. Mhe. Naibu Spika, hili tumeliona na tunakubali kwamba tutaliongezea kasi katika kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililojitokeza wakati Waheshimiwa wakichangia hapa ni pamoja na kutoa usaidizi kwa wakulima na wafanyabiashara. Wizara ya Biashara haizalishi, miongoni mwa wateja wakubwa wa Wizara hii ni wafanyabiashara wakubwa wakubwa lakini pia wafanyabiashara wale wa kati na wale wadogo wadogo. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana kabisa na Waheshimiwa kwamba ipo haja ya kutoa usaidizi kwa wazalishaji hawa na kwa kulifahamu hilo Wizara tayari inasaidia wafanyabiashara wa kati na wadogo na hapa Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano wa vikundi ambavyo Wizara ya Biashara tayari imeshaanza kutoa msaada katika vikundi hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nadhani Mhe. Salim Abdalla atakubaliana na mimi kwamba kikundi kile cha kuzalisha sabuni tumekuwa tukikitembelea sana na tumekipa msaada wa hali ya juu mpaka sasa wanaweza kuzalisha sabuni zenye viwango. Lakini bado tunaendelea kushirikiana nao ili hatimae waweze kufikia viwango hasa vya kuingia katika soko la nje ya nchi. Mhe. Naibu Spika, kuna kikundi cha Zaibat na Basma ambacho hiki nacho pia wanazalisha sabuni na wao tunashirikiana nao vizuri tunawaongezea usaidizi wa kifedha na wa kiutaalamu. Pia kuna kiwanda hichi cha chumvi kama nilivyosema kama kuna wazalishaji wale wa ndimu ambao Mkoa wa Kusini kule Chwaka na wao wapo karibu sana na wataalamu wetu kwenye Wizara yetu katika suala zima la kuhakikisha kwamba wanafikia malengo waliojiwekea katika uzalishaji wa ndimu.

Mhe. Naibu Spika, kuna hawa wazalishaji wa dagaa wa kule Ndagoni Pemba nao tumekuwa tukifanya nao kazi hizi kwa ukaribu sana kwa ushauri wa hali ya juu, lakini pia kuwatafutia soko la mazao yao ya dagaa ambayo wanayazalisha. Tumefika hadi Mhe. Naibu Spika, kuwatafutia soko nje ya Zanzibar kwa kuwasaidia kushiriki katika maonyesho yale ya Saba Saba kila pale muda unapowadia.

Mhe. Naibu Spika, katika michango mengine iliyochangiwa hapa na Waheshimiwa ni pamoja na matumizi ya ndimu ya unga. Nataka niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili Mhe. Naibu Spika, kwamba Wizara imeliona hili na imekuwa ikilifanyia kazi suala hili. Lakini pia niwatanabahishe kwamba sio tu ndio ndimu ya unga pekee iko sokoni ambayo tuna wasi wasi nayo, lakini tumegundua pia kuna aina ya kiungo ambacho kimeingia hivi karibuni katika soko la Zanzibar inaitwa anjina moto, nayo mfumo wake ukiiona ni kama ndimu ya unga, lakini watu wanasema ina ladha kwenye chakula. Sasa tuwaelimishe wananchi wetu kwamba viungo vya aina hii ambavyo vinaonekana ni vya aina ya kemikali basi kwanza tuchukue tahadhari navyo tusivutiwe tu na wale wafanyabiashara katika lugha zao lakini tuipe nafasi Wizara kufanya kazi ya kuangalia ubora wa bidhaa hizo na hasa hizi za chumvi chumvi.

Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza pia suala zima la dhana ya kutaka kubinafsisha zao la karafuu. Nadhani Waheshimiwa watakubaliana na mimi kwamba zao hili kubaki mikononi mwa milki ya serikali lina umuhimu wake. Tumeona mifano ya mazao mengi ya biashara ambayo tumeweza kusema yaingie mikononi mwa wafanyabiashara yamebinafsishwa, mfano zao la mwani. Sasa matokeo yake ni kwamba mfanyabiashara yeyote lengo lake ni ku-*maximize profit*, inapotokea kwenye soko la dunia bei ile ya zao lile ikashuka mfanyabiashara si rahisi hata kidogo kusema ngoja awasiliane na

wazalishaji wa zao lile. Lakini zaidi inakuwa baya pale ambapo bei ya dunia kule ikipanda mzalishaji huku haonekani anabakia na bei yake ile ile.

Mhe. Naibu Spika, tumeona mfano mzuri wa serikali katika kipindi cha mwaka jana katika zao la karafuu. Serikali kupitia mwenyewe Mhe. Rais alitangaza kwamba kadri ambavyo bei itakavyokuwa inapanda basi na wakulima wa zao la karafuu watakuwa wanaongezewa, lakini hata kama itakuwa inashuka kwenye soko la dunia basi wakulima wa zao lile la karafuu hawatashushiwa ile itabaki pale pale, na hapa naomba tueleweke kwamba ile tofauti huwa inachukuliwa inajaziwa na serikali kwa maana ya kwamba mfanyabiashara yeyote hawezi kuchukua hatua kama hizo. Sasa tunahofia hilo kuja kutokea kwa wazalishaji wa zao la karafuu na ndio maana utaona kwamba zao hili hatua yake kubinafsishwa bado haijachukuliwa na sidhani kama kuna hatua hiyo itachukuliwa, lengo zima ni kumlinda huyu mzalishaji wa zao hili la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, wakati wakichangia pia Waheshimiwa wamegusia suala zima la wasi wasi wao katika mezani zinazotumika upimaji wa bidhaa na zaidi za vyakula na mafuta. Zimeingia ndio Mhe. Naibu Spika, kupitia *ZSTC* mezani za *digital* bado hazijafika kwa wafanyabiashara wa bidhaa za chakula. Lakini niwatoe wasi wasi katika vipimo vya mafuta vya hivi vikopo. Mhe. Naibu Spika, hivi vikopo lazima tukubali kwamba wafanyabiashara wako wa aina tofauti lakini na uwezo wa wananchi nao pia unatofautiana. Vikopo viwepo kwa wananchi wenye uwezo mdogo lakini na vipimo vikubwa viwepo kwa wananchi wenye uwezo wa juu kidogo. Sasa hivi vikopo, Wizara yetu inafuatilia ubora wa ujazo wa vikopo hivi na kwa utaratibu maalum huwa wanapitia kwenye vituo kukaguliwa lakini pia kwa utaratibu usioeleweka wa kushtukizia ili kuona kwamba hawa wafanyabiashara hawafanyi udanganyifu katika kutumia vikopo hivi katika ujazo ule ambao umekubalika.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa mengine yaliyochangiwa na Waheshimiwa ni pamoja na hizi bidhaa chakavu au kwa lugha nyengine makachara. Mhe. Naibu Spika, suala hili Wizara inalifanyia kazi na tunakishukuru sana Kitengo cha Mazingira ambacho tunashirikiana nacho kwa karibu sana. Wizara ya Biashara kwa kuangalia ubora wa bidhaa hizo lakini kitengo hichi cha mazingira kuona kwamba bidhaa hizi haziharibu mazingira yetu ndani ya nchi kwa sababu zinaingizwa kwa wingi sana.

Mhe. Naibu Spika, kuzuia moja kwa moja uingizwaji wa bidhaa hizi kunategemea Kanuni na miongozo ambayo tayari wataalam wetu wanafanyia kazi wakisaidiana na Wizara ya Biashara na hichi kitengo cha mazingira na matokeo yake tutakavyopata kutokana na kazi hiyo Waheshimiwa hawa ndani ya Baraza lako watapatiwa taarifa hizo. Lakini pia Mhe.Naibu Spika,

pamezungumzwa suala zima la ujenzi wa vituo vya kuuzia karafuu. Tumekuwa tukijibu sana masuala hapa ndani ya Baraza lako hili tukufu kwamba suala hili tunalifanyia kazi na kutokana na uwezo wa Wizara kupitia *ZSTC* tumeliwekea utaratibu wa kuvikarabati kwa hali ya juu vituo hivi vitano kwa kila mwaka. Mwaka uliopita tulifanya kukarabati vituo vitano lakini mwaka huu nao tunakaribia kwisha nao tunakarabati vitano na mwakani tukijaaliwa vitano au zaidi ya hapo, lakini hatutoacha kukarabati vituo hivi kwa sababu sote tunaona maslahi yake kwamba ni moja miongoni mwa vituo ambavyo vinatumika katika suala zima la uchumi kwa wauzaji wa karafuu ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuitangaza Zanzibar katika maonesho. Tulishuhudia wote katika awamu ile ya Mhe. Dkt. Salmin, maonesho yale yaliyokuwa yakifanyika kule Tunguu kwa kweli yaliiletea sifa kubwa sana Zanzibar, na serikali kwa kuliona hilo tayari imeshatenga eneo kule Dimani katika Jimbo la Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni eneo kubwa tu lakini tayari serikali inajipanga kupeleka miundo mbinu ya maji, umeme na barabara ili hatimae basi tuweze kutumia eneo hilo katika kuitangaza Zanzibar kibiashara kupitia maonesho.

Mhe. Naibu Spika, mengi mengine atakuja kueleza kwa kirefu Mhe. Waziri wangu wa Biashara kwa hoja moja moja kama walivyoshauri Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu, lakini niendelee kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii basi na mimi nitamke hapa kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka huu wa fedha 2013/14 na niwashukuru sana Waheshimiwa wote kabisa ambao wametuunga mkono hotuba yetu hii na nimuombe ndugu yangu namuona sasa hivi hapa hayupo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwamba hoja yake tunaichukua kuifanyia kazi kama ambavyo tulivyokuwa tukifanyia kazi, lakini atusaidie basi kutuwasilishia bidhaa hizo ili tuweze kufanyia kazi unga huo na mchele huo mbovu ambao ameuleta hapa Barazani.

Mhe. Naibu Spika, nisema kwamba naiunga hotuba hii mkono kwa asilimia mia moja na nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu naomba kwanza kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia bajeti hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Tunaithamini sana michango hiyo kwani imetupa miongozo wa utekelezaji wa malengo yetu tuliyojipangia pamoja na kurahisisha utekelezaji wa kazi za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/14.

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu wametoa hoja zao nzito kwa heshima na hekma na busara kubwa ili tuweze kufanya kazi zetu za Wizara kwa ufanisi mkubwa na kwa lengo litakaloweza kuimarisha sekta kuu ya uchumi ambazo ni biashara na viwanda hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nachukukua fursa hii kumshukuru Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuongoza vizuri shughuli hizi na pia nachukua fursa hii kukushukuru wewe Naibu Spika na Wenyeviti wawili kutokana na juhudi yenu na kazi zenu nzuri ya kumsaidia Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi katika kuendeleza shughuli za Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Mhe. Salmin namshukuru sana yeye pamoja kamati yake yote kutokana na mashirikiano yao mazuri. Mhe. Salmin Awadhi akisaidiwa na Mhe. Hija Hassan Hija, akisaidiwa na Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, Ndg. Shemsa Maabad Mohammed na Ndg. Haji Khatib kama Katibu wa kamati. Tunawashukuru sana kwa mashirikiano yao ya dhati ambayo wametupa muda wote wa kufanyakazi nao.

Mhe. Naibu Spika, hotuba aliyoitoa Mhe. Hija Hassan Hija ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, maudhui yote ya hotuba ile tumeyachukua kama dira yetu ya kufanyia kazi katika bajeti hii ya mwaka 2013/14 na tunashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako niwataje Waheshimiwa wote ambao kwamba wamechangia katika hotuba hii ambao wote ni 16 kwa maelezo na 3 wamechangia kwa maandishi. Nitaanza kuwataja waliochangia kwa maelezo nao ni:-

1. Mhe. Hija Hassan Hija
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Subeit Khamis Faki
4. Mhe. Salmin Awadh Salmin
5. Mhe. Fatma Mbarouk Said
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Ali Abdalla Ali
8. Mhe. Asha Bakari Makame
9. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
10. Mhe. Asaa Othman Hamad
11. Mhe. Marina Joel Thomas
12. Mhe. Ashura Sharif Ali
13. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
14. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

15. Mhe. Mohamedraza Hasanali Dharamsi na
16. Mhe. Hassan Hamad Omar

Mhe. Naibu Spika, vile vile nawashukuru waliochangia kwa maandishi ambayo ni:

1. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
2. Mhe. Ali Salum Haji na
3. Mhe. Abdi Mossi Kombo

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe kwa michango yenu na tunakushukuruni kwa dhati.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla tumepokea hoja, masuala na mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe niliowataja hapo awali na nawaomba kufanya majumuisho pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja hizo kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kunisaidia kutoa ufafanuzi wa hoja nyingi sana ambapo kanipunguzia kazi na kutupunguzia muda mwingi wa kufanya kazi hii. Mhe. Hija Hassan Hija ametoa maelezo mengi sana hapa na mimi kwa kweli ninamuunga mkono sana kwamba katoa mawazo mazuri na mengi sana, lakini ninataka niseme kwamba katika kuongeza juhudi katika utafiti hasa wa mwani, hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na *UNIDO* inafanya utafiti katika zao la mwani kwa ajili ya kuongeza thamani ili kuongeza bei ya wakulima. Matokeo ya awali ya utafiti huo inaonesha kuna uwezekano mkubwa wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mwani hapa Zanzibar, kwa kuanzia baadhi ya wajasiriamali wameanza kusarifu mwani kwa matumizi tofauti ikiwemo sabuni, tutaendeleza juhudi hizi ili tutoe bidhaa nyingi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, habari ya teknolojia katika masuala ya mezani na vipimo, ushauri umechukuliwa na ni kweli kwamba mita za kupimia mafuta na mezani zinazotumia mfumo wa *digital*. Hivyo Wizara inawapatia mafunzo watendaji ili kwenda sambamba na mabadiliko haya. Mfumko wa bei za bidhaa hasa samaki, kupanda kwa bei ya samaki kunasababishwa na kukua kwa soko la utalii. Hivyo Wizara itawasiliana na Wizara ya Uvuvi ili kuongeza suala la uvuvi ili kuongeza *production* ya samaki. Utekelezaji wa matokeo ya utafiti wa dagaa, ushauri wake mheshimiwa umechukuliwa na utafanyiwa kazi lakini matokeo ya utafiti yataelekezwa ili kuzidisha sekta ya dagaa hasa katika uzalishaji (*handling*), uhifadhi (*storage*) pamoja na kutafuta soko.

Mhe. Naibu Spika, katika suala la kutenga bajeti zaidi kwa Shirika la Viwango la *ZBS* ni kweli kwamba *Zanzibar Bureau of Standard* inahitaji fedha nyingi sana ili iweze kukidhi kufanya kazi zake. Mhe. Naibu Spika, bajeti yote ya Wizara nzima hii basi kwa *ZBS* haitoshi. Kwa hivyo hiyo ni kweli lakini tunafanya jambo kwa mujibu wa uwezo tulionao.

Mhe. Naibu Spika, kufungua duka la kuuza karafuu eneo la bandarini hilo eneo tumeshalipata na hatua madhubuti zinafanywa hivi karibu karibuni tu duka hili lifunguliwe. Uzalishaji wa njugu Bwejuu namuahidi Mhe. Hija kwamba mimi mara tu baada ya kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi nitakwenda Bwejuu kutembelea watu hao ili tuweze kupanga mpango madhubuti ya nini tufanye ili kuondoa matatizo haya waliyonayo. Lakini katika mpango wa *value chain* hatutaki kuongeza thamani uuzaji wa ndimu na usarifu wake na mazao mengine ya mboga mboga, viungo, samaki, matunda, hivyo Wizara inasimamia suala la ndimu ili kuona wakulima wanapata masoko na wanafaidika na uzalishaji wa ndimu.

Bei ya mchumaji karafuu

Katika msimu wa mwaka 2011/2012 bei iliyopangwa na serikali ni shilingi 2000 kwa pishi. Bei hiyo ilizingatia mapato ya mkulima ya shilingi 15,000 kwa kila anapouza karafuu zake. Katika msimu wa mwaka 2012/2013 bei ya mkulima ilishuka mpaka shilingi 12,000 lakini bei ya mchumaji bado iliendelea kutumika hiyo hiyo bila ya kuteremshwa. Hivi sasa katika msimu huu wa karafuu bei ya *grade* ya kwanza ni shilingi 14,000 kwa kilo ambapo ni chini ya bei ya shilingi 15,000 lakini bado tunasema kwamba bei ya pishi ya karafuu ya mchumaji ni shilingi 2000 kama hapo mwanzo. Tunawaomba matajiri wote wanaochumisha karafuu wawalipe shilingi 2000 kwa pishi au zaidi, yaani bei hiyo ya shilingi 2000 isipungue inaweza kuzidi lakini isipungue. Tunawaomba wasiwadhulumu wachumaji karafuu hii kazi si nyepesi.

Maslahi ya wachukuzi Mhe. Hija Hassan Hija tunafahamu kwamba wachukuzi wanafanya kazi kubwa katika suala zima la karafuu. Hata hivyo, wachukuzi hawa si waajiriwa wa shirika, hivyo ni vigumu sana kuwapatia mafao kutoka serikalini. Kwa kuwa wao wamejiajiri na wanachama chao maalum ni vyema wakaingizwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili wapate malipo ya uzeeni. Tutawashajihisha na tutawapeleka *ZSSF* ili wasajiliwe waweze kupata mafao yao ya uzeeni kutoka *ZSSF*.

Kuhusu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk namshukuru sana kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kukusanya *samples* za bidhaa ambazo kwa mwenyewe anahisi bidhaa zile ni mbovu. Mhe. Makame Mshimba nataka nimsaidie kidogo

kwamba bidhaa zile alizozichukua akasema ni mbovu, sisi hatuwezi kuthibitisha kama ni mbovu, bidhaa zote ambazo zinathibitishwa kama ni mbovu zinathibitishwa kupitia katika Bodi ya Vipodozi na vile vile kwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Unga ukiuona mweusi au mchele mweusi au ukienda chafya hiyo haijawa sababu ya kusema kuwa unga huo ni mbovu mpaka unga huo uuchukue uupeleke katika maabara uangaliwe ili Mkemia Mkuu aseme kwamba unga huu haufai kutumiwa kwa matumizi ya binadamu. Lakini basi mimi ningemuomba Mhe. Makame Mshimba anisaidie aninong'oneze unga huu na mchele kaupata wapi, mimi nitaufuatilia kwa sababu kuna njia sahihi za kuchukua *samples* na *samples* hendi mtu akanyakua tu kama anayechuma chungwa, kuna vifaa vyake vya kuchukulia *samples* na kuna njia zake na namna ya kuzi-*handle* mpaka kufika katika maabara na kufanyiwa uchunguzi. Kwa hivyo, kuona kitu kibovu ni suala moja lakini kuchunguza na kuthibitisha ubovu wa bidhaa hiyo ni suala jengine na ni suala muhimu sana.

Mhe. Makame Mshimba tunakushukuru sana na tunataka ushirikiane na sisi kila wakati unapoona bidhaa mbovu utuletee habari hiyo. Tunawashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kutupa habari mara kwa mara kwa njia ya simu au njia ya *message* au kuja wenyewe kutwambia wanapohisi kuna bidhaa mbovu katika maduka na sisi hufuatilia na kuona kwamba tunachukua hatua gani ya kuzifanyia uchunguzi na kuwachukulia hatua wale wote ambao wanauza bidhaa mbovu.

Mhe. Mshimba vile vile alitaka kujua maeneo yaliyoanza kilimo apewe mwekezaji wa Kiwanda cha Maziwa. Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Mshimba kwamba mradi wetu wa maziwa unaitwa *Azam Diaring Products Factory*, mwekezaji wa kiwanda hiki ni ndugu yetu Said Salim Bakhressa na mradi huu utagharimu dola za Kimarekani milioni 19.34. Mradi huu uko katika eneo la Fumba na katika eneo hilo amepewa hekta saba na ameshaanza kazi na kazi hii ya ujenzi imefikia asilimia 70. Vile vile Ndugu Said Salim Bakhressa amejenga huduma nyingi za miundombinu, kwa hivyo amesaidia sana ni mwekezaji mmoja wa awali aliyewekeza katika eneo hili kwa ufanisi wa hali ya juu na anastahiki pongezi nyingi sana na ndio maana nikampongeza katika hotuba yangu niliyoisoma jana.

Katika eneo la Fumba kiwanda hicho kitajengwa na vile vile soko la kiwanda hiki litakuwa Zanzibar, Tanzania Bara, Afrika Mashariki, *SADC* na nchi za mbali. Kwa hivyo, hiki ni kiwanda kikubwa kitakachotoa aina mbali mbali za bidhaa zinazotokana na maziwa. Ajira ya moja kwa moja katika kiwanda hiki kitaajiri waajiriwa 100 katika kiwanda lakini waajiriwa wengi wataajiriwa nje ya kiwanda hiki. Mradi huu utaanza kazi zake katika mwaka 2014 na Ndugu Said Salim Bakhressa ameshalipa *compensation* zote za kiasi cha shilingi

65,305,500 na mradi wa kufuga ng'ombe tunatarajia pengine utakuwa katika sehemu za Kizimbani.

Ninalowaambia ndugu zangu wananchi kwamba mradi huu utapata faida kubwa sana kwani Mhe. Said Salim Bakhressa ng'ombe wengine atawapa wakulima wafuge ambao kwamba maziwa yake moja kwa moja atanunua mwenyewe na atakuwa na madaktari wa kushughulika na ng'ombe hao na baada ya miaka mitano wanachinjwa na nyama yao ni laini kama sufi. Kwa hivyo, naamini kwamba kuja kwa kiwanda hiki Zanzibar kutatoa fursa nyengine zaidi kama ile ya karafuu ya kuwasaidia wafugaji wa ng'ombe na itasaidia wafanyabiashara. Tumuombee dua Ndugu Bakhressa aweze kukamilisha mradi huu kwa vizuri. Zaidi ya hayo nataka tuwaombe wananchi wa Zanzibar tumkaribishe ndugu yetu Bakhressa, mwekezaji huyu ana nia ya dhati na nia nzuri ya kuendeleza Zanzibar. Mwekezaji huyu anatakiwa Congo, Rwanda, Kenya, Afrika ya Kusini, anatakiwa dunia nzima, tukimbeza sisi, hapa kwao tutamkosa. Kwa hivyo, ni lazima tumpe mashirikiano ya dhati ili aweze kuja kuwekeza zaidi na zaidi Zanzibar, nia yake ni nzuri lakini anahitajia tumuunge mkono na hasa sisi Wawakilishi humu ndani. Wajasiriamali wapewe nyenzo bora ambapo Mhe. Mshimba nazungumza suala hilo, tutalifanyia kazi na tutahakikisha kwamba wajasiriamali tunawatumikia.

Suala la viwango vya mafuta katika kudhibiti ubora wa mafuta. Mhe. Mshimba kweli mafuta yanayokuja hasa Pemba yanaleta athari kubwa sana katika magari yetu, hata gari yangu kule Pemba ya Wizara ya Biashara ilikufa muda wa mwezi na nusu nafika pale njiani nakwenda *airport* gari ikasimama kumbe matatizo mafuta, mafuta yanayokuja hayana viwango. Nakuhakikishieni kwamba *ZBS* inaanza kazi zake na moja katika tutalofanya ni kuyakagua mafuta yanayoingia Zanzibar, lazima yakidhi viwango na yoyote ambaye ataleta mafuta ambayo hayakidhi viwango akituharibia magari yetu tutamchukulia hatua za kisheria. Kwa hivyo, Mhe. Mshimba nakuhakikishia kwamba wizara hii itafanya kazi zote hizo tulizozisema kwa moyo mkunjufu kabisa na itashirikiana na wewe kuona kwamba pale pahala penye chakula kibovu inashughulikia ipasavyo. Ukaguzi wa bidhaa utazidi kufanywa kwa nguvu zaidi.

Mhe. Subeit Khamis Faki tunakushukuru sana kwa maelezo yako na umetupa ushauri mzuri sana na tutauchukua. Nataka nikuhakikishie kwamba *ZSTC* inatoa huduma za mikopo na vifaa kwa wakulima, kwa ajili ya kuvuna karafuu na wale wote wanaotimiza masharti ya mikopo hiyo hupatiwa bila ya pingamizi yoyote. Kwa hivyo, wale wote ambao wanataka kukopa majamvi, wanataka mambo mengine yote wafike *ZSTC* na tumeshajitayarisha ili kuwahudumia wakulima na wachumaji wa karafuu ili wazipate karafuu zenye

sifa na ubora wa hali ya juu. Suala la mwani nimeshalieleza kwamba tunalishughulikia na tunataka kuona kwamba wakulima wa mwani wanafarijika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin serikali iongeze bajeti ya wizara, kweli tumepata bajeti ndogo lakini ndio hali halisi ilivyo na tunakushukuru sana kwa kutuombea kuwa bajeti iongezwe Waziri wa Fedha yupo amekusikia.

Mafuta ya kupikia ambayo yamepigwa marufuku Tanzania Bara ambayo hutumika Zanzibar. Hili amelieleza Mhe. Salmin Awadh na amefafanua zaidi Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Salmin na Mhe. Jussa naomba niwahakikishie kwamba wizara yangu imeshughulikia kwa upeo mkubwa kuhusu suala hili na kwamba nimepokea au nimepata malalamiko mengi na barua rasmi kutoka kwa *Zanzibar National Chamber of Commerce Industry and Agriculture* (*ZCCA)* yenye *reference No. ZCCA WBPM 18/38 Volume* 44 ya 1960 ya tarehe 29 Julai mwaka 2013 inayoeleza kadhia ya kupiga marufuku mafuta ya *OKI*, *Viking* na Asma.

Katika barua hiyo ambayo ina vielelezo mbali mbali inaonesha wazi kwamba *TBS* inatumiwa na baadhi ya wafanyabiashara na inakiuka ile hasa jukumu lake ililopewa na Serikali ya Tanzania la kumlinda mlaji, badala yake sasa hivi *TBS* inawalinda wafanyabiashara, inalinda maslahi ya biashara. *TBS* haitumiki kuwalinda wananchi wa Tanzania kwa kweli inatupa sura mbaya kabisa. Naomba niwahakikishie Wazanzibari wote kutokana na uchunguzi uliofanywa na Mrajis wa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kwamba mafuta ya *OKI*, *Viking* na Asma hayana matatizo yoyote. Wazanzibari msiwe na wasi wasi na mafuta haya, mnunue na myatumie chombo chetu cha uchunguzi cha Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kimenithibitishia kwa barua na kimehakikisha mara tatu kuangalia vifaa hivyo kwamba mafuta hayo yanafaa kwa kutumia binadamu, naomba msiwe na wasi wasi wowote mtumie mafuta hayo na tunahakikisha kwamba mafuta haya ni mazuri tu. Huu ni ukiritimba wa kibiashara ambao unafanywa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Salmin nakuhakikishieni kwamba nimempigia simu mwenyewe Waziri wa Biashara wa Tanzania Mhe. Abdalla Kigoda nimemwambia kwamba nina ushahidi suala la mafuta halikwenda kwa mujibu wa sheria ya *TBS*. Ni kwamba *TBS* inatumiwa kama nyezo moja ya kudhoofisha biashara kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam. Nikamwambia Mhe. Kigoda kwamba wafanyabiashara hawa kwanza walitumia *TRA* kuzuwia bidhaa hizi, majahazi kutoka Zanzibar kama alivyosema Mhe. Mohamedraza Hassanali hapa yalitoka Zanzibar na *Tranzaya ya Metrashipment* yana fomu za *TRA* yanakwenda zake Dar es Salaam. Kama alivyosema Mhe. Raza yalipofika njiani kuna boti ya *TRA*

ikazikamata boti zile jahazi zinatoka mbali na zikaanza kuadhibiwa *Dhwaarban Shadida*. Haya ambayo Mhe. Raza ameyasema ni ya kweli na kuna tetesi kwamba wafanyabiashara hawa wametoa shilingi milioni saba kila jahazi moja iliyokamatwa ili kuwapa zawadi *TRA*. *TRA* wamefanya kazi hiyo mpaka walipochoka wakayaacha sasa hivi wafanyabiashara hawa wameona njia moja nyepesi ya kutumia ni kutumia *TBS* ili iwafanyie kazi yao.

Wafanyabiashara hawa wana viwanda vya mafuta Dar es Salaam lakini wanatumia mafuta hayo kutoka Malaysia na nchi nyengine za nje si mafuta kutoka Tanzania, si mafuta ya Mwanza, si mafuta ya Shinyanga, haya ni mafuta kutoka nchi za nje Malaysia na nchi nyengine. Na inasemekana mafuta haya ni *semi processed*, si *crude oil*. Kwa hivyo, wanatudanganya, wanatumia *TBS* kudhoofisha biashara ya Zanzibar.

Mimi kama Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko sikubaliani kabisa na mtindo huu wa kidhalimu. Nitafanya juhudi yoyote ile kusimamia na kuona kwamba wafanyabiashara wa Zanzibar hawadhalilishwi. Nilimwambia Mhe. Kigoda kwamba tutagawana mbao kabla ya kumaliza hili suala la Katiba na Mhe. Kigoda amenihakikishia kwamba suala hili atalishughulikia ipasavyo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said ameeleza suala la *taskforce*. Mhe. Bi. Fatma suala la *taskforce* najua kwamba litakutia shida sana kwa sababu hujalijua undani wake. *Taskforce* hizi zimeundwa miaka mingi, katika historia tangu miaka ya nyuma *taskforce* Mhe. Rais anaunda wakati wa karafuu na kwa muda mrefu *taskforce* ilikuwa hamna na ndio maana masuala ya magendo na masuala ya udhibiti wa zao la karafuu ukawa dhaifu mno. Kwa hivyo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona umuhimu wa zao la karafuu na kuzuia magendo aliona hakuna budi isipokuwa iundwe *taskforce*. Kwa nini *taskforce* ikaundwa? Magendo ya karafuu nyingi zinakwenda Kenya sio tu kuondosha ile mali ya Zanzibar, lakini inatoa taswira mbaya ya zao la karafuu. Karafuu inapokwenda kuuzwa nchi za nje kwa jina la Zanzibar zilikuwa mbaya sana zimeharibiwa (zimechakachuliwa) vibaya sana na zinaharibu jina la Zanzibar. *Taskforce* hii ina wajumbe muhimu sana ndani yake, ina makamanda wote wa vikosi vyote vya ulinzi nchini, ina Wakuu wa Mikoa wote, ina Daktari Mkuu, Mkurugenzi wa Wizara ya Afya Dr. Malik, ina Naibu Mwanasheria Mkuu, vile vile ina *DPP*. Kwa hivyo, hii ni kamati *very strong* na inafanya kazi vizuri sana.

Mhe. Fatma Mbarouk hili suala la ulinzi ni katika kila kampuni. Kampuni yoyote ya biashara ni lazima iwe na ulinzi na kama haina ulinzi basi mali hupotea bila ya habari. Kwa hivyo, hii *taskforce* imefanya kazi ya ulinzi mkubwa sana na ndio chachu ya kuweza kufanikiwa kupata karafuu zaidi ya

tani 4,500 na kuweza kupata mafanikio makubwa. *ZSTC* inapata mafanikio makubwa sana kutokana na msaada wa *taskforce*.

Pesa ambazo *taskforce* katumia kutokana na kazi hiyo ni asilimia ndogo sana, ni 0.001 yaani ni magunia 40 tu ya karafuu, thamani yake iliyotumika katika kufanya kazi hiyo lakini tumeweza kuhifadhi zaidi ya shilingi bilioni 35 kutokana na kazi za *taskforce*. Kwa hivyo, nataka kukutoa wasi wasi Mhe. Bi. Fatma kwamba tumefanya kila aina ya jitihada *taskforce* inafanya kazi vizuri sana na inabidi kupongezwa na ni bora tuiachie iendelee.

Mhe. Fatma vile vile alisema *ZSTC* kuna wafanyakazi hawa wakistaafishwa itakuwa vibaya na hivi na hivi. Mhe. Fatma nakuhakikishia kwamba wafanyakazi hawa wanaacha kazi wakiwa katika hali ya furaha na wenyewe wameridhika. Mhe. Fatma Mbarouk nikikwambia sasa hivi imebaki miaka miwili wewe kumaliza kazi zako za uwakilishi, kakae nyumbani nakupa mshahara wako wote wa miaka miwili, nakupa na marupurupu yako yote ya miaka miwili utayakataa Mhe. Fatma? Huwezi kukataa, kwa sababu tunakupa nafasi nyengine ya kwenda kujiimarisha na maisha yako hatukuondoi sisi mkavu mkavu, unaondoka mzuri hali ya kuwa mwenyewe umeridhika. *ZSTC* sasa hivi ina wafanyakazi 157 na 12 walistaafu wenyewe na muda wao ukifika lakini 61 wanastaafishwa kama nilivyosema kwamba na mafao yao ni karibu shilingi 2.8 bilioni. Hii inatokana na kwamba wafanyakazi hawa kwa sasa hivi hawana kazi ya kufanya katika *ZSTC* wamekaa kitako, zile kazi za kufanya hazipo ndio maana tukawastaafisha. Lakini tunahitajia wafanyakazi wenye utaalamu wa hali ya juu ambao sasa hivi tisa tumeazima kutoka katika sehemu nyengine za serikali. Kwa hivyo, Mhe. Fatma Mbarouk usiwe na wasi wasi wote hawa tunathamini michango yao na kwa kweli walikuwa wanafanya kazi nzuri.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu suala la mafuta nimelielezea kwa urefu na ushauri wake kwenye uwanja wa maonesho na ninauchukua na nitaufanyia kazi. Ni kweli *thesis* hii ni muhimu sana na kama nilivyosema kwamba inahitaji fedha nyingi kumaliza mchakato wake. Kwa hivyo, tumo katika kudowea fedha zikipatikana tu ripoti nzuri ya *thesis* itakuja katika Baraza la Wawakilishi na tutapata michango ya Wawakilishi wote.

Habari ya maonesho kweli ni faraja muhimu sana na Dr. Salmin Amour alianza na mimi nilikuwa kama kiranja wake wakati ule na tulifanya kazi nzuri sana. Lakini pia kwa sasa hivi tunaifanyia kazi na *Inshaallah* mwakani tutapokuja tutakuja na ripoti nzuri sana. Kwa hivyo, uwanja wa maonesho ni muhimu, *thesis* ni muhimu Mhe. Jussa ushauri wako ni mzuri na tunaufanyia kazi.

Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Madawa nayo ofisi yangu inalifanyia kazi katika suala la kumaliza eneo la Darajani. Kweli kuna bidhaa nyingi Darajani zinatupwa tupwa tu pale nyingi sana. Hata mimi mwenyewe juzi nimekwenda nimenunua baadhi ya bidhaa kwa kuzifanyia uchunguzi, sikumtuma mtu nimekwenda mwenyewe nimeziona bidhaa nyingi sana na nimewahoji wale. Bidhaa zile hawakuagiza wao, wao wamezitoa katika maghala ya wafanyabiashara wakubwa, vitu ambavyo vinakaribia ku-*expire* wanawapa ndio wanakuja kuuza pale kwa bei rahisi ili wasafishe maghala yao. Kwa hivyo, uchunguzi tunaufanya na atakayebainika kwamba anatumia fursa hiyo ya kuwauzia watu bidhaa mbaya tutawachukulia hatua zinazofaa. Kwa hivyo, tunakushukuru sana Mhe. Jussa umetuamsha hilo tumeliona lakini umezidi kutupa moyo kwamba kumbe hili si suala la Wizara ya Biashara peke yake ni suala la wananchi wote wa Zanzibar, wasikubali kununua bidhaa mbovu, wasikubali kuuziwa vitu vilivyopitwa na wakati na Wizara ya Biashara iko tayari kusikiliza maoni yao wakati wowote wapige simu, wafike ofisini watuelezee na tutachukua hatua inayostahiki.

Maghala yalioko katiak Mji Mkongwe suala hili linazingatiwa na ni kweli maghala ya Mji Mkongwe yapo kama ilivyokuwa enzi za zamani. Hapo zamani Mji Mkongwe maghala yalikuwa mengi sana lakini wakati ule maghala haya yalikuwa yakitumia marikwama, kulikuwa na marikwama marefu ya tani tano, tani mbili na tani moja. Sasa hivi marikwama hakuna tena basi magari yanaingia ndani na imekuwa ni bughudha katika Mji Mkongwe na inaweza kuhatarisha kuvunja nyumba za Mji Mkongwe. Kwa hivyo, masuala ya maghala tutawasiliana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati itoe viwanja maalum vya kujenga maghala, tutawasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ijenge barabara ili wafanyabiashara wapewe *site* nzuri ya kujenga maghala na barabara ijengwe ili magari hayo yafike kwa wepesi katika sehemu ya maghala hayo ili ipatikane nafasi nzuri katika Mji Mkongwe. Huu ni mji wa kuenziwa, huu ni mji muhimu sana kwetu kwa sababu unatupa faida kubwa sana katika masuala ya utalii na masuala ya kujenga *heritage* ya nchi yetu.

Mhe. Ali Abdalla Ali kwa kweli tunakubali kwamba miche ya mikarafuu ni muhimu sana na sisi tunashirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili tunafanya kazi nzuri sana ya kutafuta miche ya mikarafuu ili kuongeza zao hili liweze kuimarika. Sasa hivi zao hili limezidi kuwa chini kama nilivyosema na tutafanya kazi nzuri sana.

Vituo vya karafuu vya Dubai na Dar es Salaam, ni kweli Dar es Salaam kuna duka letu na Dubai kuna duka letu. Kwa muda mrefu vituo hivi havijafanya kazi nzuri, ni kweli na kila mtu anaona kama havina maana lakini kwa mkakati wetu tuliopanga wa kuuza karafuu baada ya kufanya *brand* soko la

Afrika Mashariki toka Tanzaia itategemea sana kuwa ofisi yetu ya Dar es Salaam itafanya kazi nzuri sana. Vile vile katika soko la Jordan, Oman, Iran, Saud Arabia na wenziwe wote wa Mashariki ya Kati itafanya kazi sana, ofisi yetu ya Dubai. Kwa hivyo, nakuomba utustahamilie tumalize suala la *branding* ili tuweze kuuza bidhaa zetu kwa kutumia ofisi mbili hizi ambapo zitafanya kazi zake nzuri sana.

Mheshimiwa tunakubali umeme ni ghali sana na Mhe. Waziri wa Fedha anafanya kazi nzuri sana ya kutafuta wawekezaji ambao wataweka nishati kwa bei nafuu. Kwa hivyo basi usiwe na wasi wasi Waziri wa Fedha anafanya kazi nzuri.

Kuhusu vitu chakavu wizara itashughulikia suala hili kwa kuwekwa viwango, hatuwezi kuchukua vitu vilivyokwishapitwa na wakati bila kiasi lazima tuweke *quality* hata ikawa ni *used* basi ni *used* ya *quality* sio mataka taka. Kwa hivyo, wizara hii itafuatilia suala hilo na suala la *samples* za mafuta yanayochakachuliwa tutayafanyia kazi Mhe. Ali Abdalla.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali suala la *bar-code.* Faida ya *bar-code* ni kutafuta bidhaa katika masoko ya ndani na nje. Kwa hivyo, Mheshimiwa *bar-code* ni muhimu sana kama *bar-code* hatuna kutakuwa hakuna *feasibility* na kwa kweli tangu kuanzishwa *bar-code* tumepata mafanikio makubwa sana Mhe. Abdalla Mohamed.

Dawa za sabuni za vyoo zimepata soko kubwa sana, hizi dawa zinatoka Pemba lakini zimepata masoko katika Dar es Salaam. Vile vile *herbal* zimepata masoko sehemu za Rwanda na hizi zinatoka Nungwi, *from* Nungwi zimekwenda mpaka Rwanda kutokana na hiyo *bar-code*. Sabuni hizi za *spices* vile vile zimepata soko kubwa kutokana na *bar-code.* Kwa hivyo, *bar-code* ni suala muhimu sana wala tusilidharau.

Kiwanda cha Sukari Mahonda Mhe. Abdalla Mohamed na Mhe. Ashura walikuwa wameuliza suala la Kiwanda cha Mahonda. Nataka niwape habari kiwanda cha Mahonda kweli sijajua mimi kama kuna mashamba ambayo yamevurugwa mashamba ya mpunga. Hili nitalifuatilia kupitia kwa Mkuu wa Mkoa na tutaangalia nini itakavyoelekea. Lakini nataka niwaambie kwamba katika jitihada za wenyewe Kiwanda cha Mahonda ni kwamba kimepanga mpango wa mwaka 2013/2014. Sisi serikali tumefanya mpango wa kutaka kuuvunja mkataba huu lakini tunakwenda kwa mujibu wa sheria, lakini mwenyewe huyu mwenye kiwanda na yeye anafanya mpango ambao naona mimi mpango huu ni mzuri na mimi naona unaweza kuzaa matunda.

Kiwanda hiki kimejipangia mpango wa mwaka 2013/2014. Sasa hivi kuna miwa tayari ya kuvunwa mwaka huu kwenye eneo la ardhi la ekari 1,600. Wanatarajia kutoa sukari katika mwezi wa Disemba mwaka huu sukari tani 2,500 sawa na magunia 50,000. Katika mwaka 2014/2015 watapanda miwa katika ekari 3,250 itatoa magunia 10,000 na itatoa magunia laki mbili, katika mwaka 2015/2016 italima ekari 3,900 na itatoa magunia ya sukari 260 elfu na tani 13 elfu. Kwa hivyo ukiangalia katika mambo yao kiwanda hiki sasa hivi kinafufuliwa kwa sababu mwekezaji mpya ameingia kumuunga mkono mwekezaji aliyepita *Shanter Sugar* kutoka India ambaye anashirikiana na *East African Trading (EAT*). Kwa hivyo, tunaangalia kampuni hii kwa jicho kali kabisa kuona kwamba ikishindwa kuweza kututekelezea kwa mujibu wa huo mpango waliopanga basi serikali itaendelea kuchukua hatua yake kama kawaida.

Vile vile *Spice Island* anasema Mheshimiwa jina la *Spice* lifutwe. Nasema jina hili lisifutwe jina hili ni la asili, jina hili linafanyiwa kazi, *spices* tunazipanda na nyengine tutaziagiza. Dubai inaitwa *City of Gold* wakati Dubai hakuna mgodi hata mmoja wa dhahabu, lakini Dubai ni *city of trade* na Zanzibar ni *island of trade*. Kwa hivyo, *spices* bado jina hili ni muhimu na itabidi likae katika suala hili.

Habari ya maghala *full security* naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba suala la *full security* halipo katika Wizara yetu ya Biashara, suala hili liko katika Wizara ya Kilimo na Maliasili lakini sisi tunaangalia namna gani wafanyabiashara wanaingiza bidhaa hizi katika maghala yao isipungue. Kwa mfano, katika mwaka 2012 mchele ulioingia nchini ni tani 91,729 ambao kwa kweli sisi tunahitajia tani 60,000 tu. Kwa hivyo, tulikuwa na akiba ya mchele mwingi sana katika mwaka wa 2012. Unga wa ngano tulikuwa na akiba karibu tani 3,000 na sukari tulikuwa na akiba karibu tani 30,000. Kwa hivyo, katika mwaka 2012 tulikuwa na akiba kubwa ya chakula inayofikia tani 170,000/-. Kwa hivyo, nakushukuru sana lakini suala hili limo katika wizara ya nyengine ya kilimo.

Mhe. Asaa Othman Hamad bidhaa feki *ZBS* itaandama yoyote atakayekuwa na bidhaa feki, sheria itachukua mkondo wake. Nishati ghali ni kweli lakini kama nilivyosema inafanyiwa kazi. Vile vile naomba Bi. Ashura nimeshakujibu suala lako, Mhe. Asaa Othman nimeshakujibu suala lako na kwa kweli nawashukuru wote ambao wamenisaidia.

Mhe. Mohamedraza kuna suala lake muhimu sana alilolieleza pale habari ya *agent*. Ni kweli kabisa kwamba hapa sisi tuna serikali mbili sasa hivi, Serikatli ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali ya Tanzania inashughulika na *all union matters,* Serikali ya Zanzibar

inashughulikia *all union matters*. Serikali ya Zanzibar inashughulikia na *all non-union matters*. Wizara ya Biashara haimo katika *union matters.* Kwa hivyo, Wizara ya Biashara moja kwa moja inashughulikiwa na Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa hivyo, kuwanyima fursa ya uajenti wafanyabiashara wa Zanzibar ni kuwaonea. Kwa hivyo, Wizara yangu tangu mwaka jana suala hili tumelichukua tunalifanyia kazi kuona kwamba lazima tugawane. Sasa hivi maajenti walioko Dar -es Salaam wale wale na Zanzibar wapewe uajenti vile vile. Uajenti usiwe wa Tanzania Bara tu. Lazima uajenti uwe wa nchi mbili, mmoja uweko Zanzibar na mwengine uweko Tanzania Bara, isiwe uajenti ule wanauhodhi peke yao.

Hilo ni kweli na nitalifanyia kazi Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali na *inshaallah* katika kipindi kifupi kijacho kutoka mazungumzo yangu na Wizara ya Biashara Tanzania Bara naona tutafikia muafaka kuona kwamba tunagawana masuala haya na Zanzibar na sisi tunachukua ajenti kama wao. Kwa hivyo, itakuwa nchi moja *system* ya biashara ziwe mbili.

Suala la *COMESA* tutalifanyia kazi, *East African Community* tunashiriki kikamilifu sote na tunalinda haki yetu ya Zanzibar. Nataka kuondoa wasi wasi maana mmoja kasema mnapata faida gani nyie katika vikao hivi. Nasema tunapata faida kubwa sana kwa sababu sisi tusiposhiriki katika vikao hivi vya *East African Community* tukishiriki katika vikao vya *SADC* tunainyima fursa Zanzibar kuekeza mkono wake katika masuala ya ushirika huu. Kwa hivyo, tunakwenda sambamba na wenzetu Tanzania Bara kudai haki za Zanzibar kwa sababu biashara ni suala la Zanzibar, si suala la Muungano.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na nawashukuru sana Wawakilishi wote kwa kuniunga mkono sana na kunipongeza sana. Pongezi zao mimi zinanipa fursa na zinanipa nguvu mpya kabisa naondoka hapa nikiwa na nguvu kubwa kabisa, nikiwa na kasi kubwa kabisa, nikiwa na ari kubwa kabisa ya kufanyakazi katika mwaka 2014 *Inshaallah* mnisaidie na naomba Mwenyezi Mungu anisaidie. *Wabilahi Taufik.* Naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale waliokubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa mwaka 2013/2014 wanyanyue mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda (*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuingia katika kamati nilikuwa na ushauri kama tutakubaliana naomba tuufate. Kwa kuwa muda wetu umebakia dakika 25 tuongeze kabisa muda mpaka saa 6:20 ili tumalize moja kwa moja. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais afanye utaratibu. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa leo ni Ijumaa na sasa ni saa 5:30 na kwa kuwa tunataka kupitisha Bajeti yetu ya Wizara ya Biashara, hivyo niliombe Baraza lako Tukufu liweke muda wa kanuni zetu kando ili tuweze kumaliza shughuli zetu hizi saa 6:30 barabara leo ili tuwahi msikitini. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikia)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 21- WIZARA YA BIASHARA VIWANDA NA MASOKO

Kifungu 0601 -	Idara ya Biashara	90,000,000/=
Kifungu 0301 -	Ofisi Kuu Pemba	346,950,00/=
Kifungu 0401		

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, lakini kuhuwepo tulipokuwa tukipitisha majumuisho.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimendika haya majibu nilikuwepo kwenye redio na nimeandika jinsi alivyojibu sina haja ya kufungua.

Mhe. Naibu Spika: Sisi tutajuaje kama uko kwenye redio. Tupe ushahidi wa kuwa ulikuwepo kwenye redio.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nasemaje Mhe. Mwenyekiti….

Mhe. Naibu Spika: Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu 0401 -	Idara ya Mipango na Sera	372,950,000/=
Kifungu 0501	Idara ya Viwanda	260,900,000/=
Kifungu 0601		

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati nna nia njema nimeunga mkono hotuba. Lakini nilitaka maelezo kidogo nilichangia kwa maandishi na kwa bahati mbaya kwa sababu ya ku-*save* muda sikuwahi kupata jawabu hata dogo. Sasa Mhe. Waziri nilimuuliza suala dogo sana tu. Kuna wafanyabishara wanaouza samaki pale Amani/Tigo na mpaka kweye vyombo vya habari tumesikia jana walilalamika eneo lao kuchukuliwa na mfanyabishara mwengine na Wizara ya Biashara inapiga kelele kuwatafutia wafanyabiashara maeneo ya kufanyia biashara.

Sasa nilitaka nipate maelezo tu nani amechukua na kwa utaratibu gani Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biasharas Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipata karatasi yake anataka kujua wafanyabiashara wale wa Amani/Tigo. Kwa bahati mbaya mimi ni Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko kweli lakini haya masoko ya kuuzia bidhaa kama Soko la Darajani, Mwanakwerekwe au Magenge si kazi yangu ni kazi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hata hivyo ile karatasi nimempa kijana wangu amekwenda kufuatilia suala hilo. Mimi sipendi kujibu suala ambalo silifahamu wala silijui. Kwa hivyo, kijana nimemtuna ili ende akaangalie kama ni kweli tulifanyie kazi.

Ninamuahidi kwamba mimi pamoja na Mhe. Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi suala hili tutalishughulikia kwa sababu hawa ni wananchi wetu na hatutaki wanyanyaswe. Kwa hivyo, tunalifanyia kazi mimi na wewe na Mhe. Waziri ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri majibu yake na niseme tu hiyo ndio kazi yetu. Wafanyabishara ni lazima tuwajali na lazima tuwatatulie shida zao na imani yangu kwamba panapotolewa eneo na nasikia eneo lile lilitolewa kwa wafanyabiashara akina mama.

Sasa wao wakifuatilia watajua zaidi na dhamira ya kutolewa kitu kinatolewa kwa lile lengo lililokusudiwa. Sasa kama kuna watu kama wameliuza kwa lengo ambalo halikusudiwi. Naomba niwaachie mawaziri hawa wawili walifuatilie ili tuwasaidie akinamama wa eneo lile. Mhe. Naibu Spika, tuendelee.

Kifungu 0601	Idara ya Biashara	13,000,000/=
Kifungu 0701	Utumishi na Uendeshaji	1,192,200,000/=
Kifungu 0702	Baraza la Biashara Zanzibar	300,000,000/=
Kifungu 0703	Mamlaka ya Mizani na Vipimo	100,000,000/=

Kifungu 0704	Kamisheni wa Kusimamia Ushindani wa Biashara	150,000,000/=
Kifungu 0705	Mamlaka ya Viwango Zanzibar	600,000,000
Jumla ya Fungu		**3,690,000,000**

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	930,000,000/=
Kifungu 0501	Idara ya Viwanda	220,000,000
Kifungu 0601	Idara Biashara	150,000,000
Jumla ya Fungu		**1,300,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa tukae. Mhe. Waziri. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko yoyote, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba niwashukuru kwa kazi nzuri tulioifanya hasa leo.(*Makofi*).

TAARIFA

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba utuongoze kwa sababu ulituomba mpaka saa 6:20 na hatukumaliza kutokana na *speed* ya Waziri. Naomba utuongoze uturuhusu tuendelee na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kazi ya leo tumemaliza na kazi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tumekusudia tuanze kesho. Kwa hivyo, kiti kina ruhusa ya kuahirisha kikao hichi.

Lakini kabla ya kuahirisha nina tangazo nimepewa na Mwenyekiti wa UWAWAZA kwamba Waheshimiwa wanawake wote tukimaliza kikao hichi wabakie kwa dakika mbili kuna jambo muhimu.

Baada ya maelezo hayo naomba sasa kuahirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Jumamosi tarehe 03/08/2013 saa 3:00 asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 6:15 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 03/08/2013 saa 3:00 asubuhi)